Gazeti la kwanza la Kiislam kutolewa kwa lugha ya Kiswahili - mwaka 1936

Mapenzi ya Mungu

Mapenzi kwa wote bila chuki kwa yeyote

DAR ES SALAAM TANZANIA

Nukuu ya Qur'an Tukufu

"Ewe Nabii, kwa yakini Sisi tumekutuma (ili uwe) shahidi na mtoaji wa habari nzuri, na Mwonyaji.
Na mwitaji (wa watu) kwa Allah, kwa idhini Yake, na taa itoayo nuru.
Na uwape habari njema waaminio ya kwamba wana fadhili kubwa itokayo kwa Allah " (33:46-48).

JUZU 77 No. 192 | RAB. II - JUM. I 1439 AH | JANUARI 2018 | SULHU 1397 HS | BEI TSH. 500/=

Khalifa Mtukufu awakumbusha Waislamu kutangaza kwa matendo:

Mtume s.a.w. ni Rehema kwa Ulimwengu

Na Mwandishi Wetu

Katika hotuba ya Ijumaa ya tarehe 01 Disemba 2017, Hadhrat Amir-ul Muminiin, Khalifatul Masih V a.t.b.a. alisema kwamba kumbukumbu ya kuzaliwa kwa Mtume s.a.w. itumike katika kutangaza sifa ya Rehema ya Mtume s.a.w.

Baada ya Tashahhud, Taa'udh na Surat Fatihah Hadhrat Amir-ul Muminiin (atba) alisema:

Mwezi 12 wa Rabi al - Awwal ni siku ambayo Mtukufu Mtume s.a.w alizaliwa. Alishatajwa kuwa ni taa inayoangaza mwanga mkali ulimwenguni kote kwa mwanga wa kiroho. Kuhusu yeye ambaye Allah Mtukufu alisema, "Nasi Hatukukutuma ila uwe rehema kwa Ulimwengu" (21:108) Mafundisho yake ni rehema kwa kila mtu hadi siku ya Kiyama. Allah Mtukufu aliwaambia wafuasi wake kuwa Mjumbe huyu wa Allah ni mfano bora kwenu kama alivyofafanua kuwa "Bila shaka mnao mfano mwema katika Mtume wa Allah, kwa mwenye kumwogopa Allah na siku ya mwisho na kumtaja Allah sana." (33:22).



Sehemu ya waumini ndani ya Baitul Futuh, msikiti uliopo jijini London ambao Hadhrat Khalifatul Masih V a.t.b.a. hutoa hotuba zake za Ijumaa na kurushwa duniani kote kwa njia ya satelaiti.

Mtume wetu s.a.w. alitufafanulia njia za kuweka Umoja wa Mungu, ibada na maadili bora ya kutimiza haki za wanadamu. Ingawaje, mwenendo wa Waislam wengi ni kinyume kabisa na mfano wake.

Mwezi 12 wa Rabi al-Awwal, badala ya kusambaza ujumbe wa huruma na wema mbalimbali wa Mtume s.a.w, Umma wa Kiislam umejawa na fujo na machafuko. Hali ni mbaya sana huko Pakistan ambapo huduma za simu kwa baadhi ya miji ya Pakistan zimetakiwa kufungwa leo hii na kuna ulinzi mkali kila sehemu. Wanawafedhehesha

Endelea uk. 3

Shani ya Jalsa Salana 2017 kupitia vyombo vya habari

Na Jamil Mwanga

Mkutano wa mwaka (Jalsa Salana) ni tukio adhimu la kidini katika mustakbali ya Jumuiya ya Waislamu Waahmadiyya. Mkutano huu ulianzishwa na mwanzilishi Mtukufu wa Jumuiya ya Waislamu Waahmadiyya Hadhrat Mirza Ghulam Ahmad a.s. kwa lengo la kukuza Imani, kujiongezea maarifa na elimu ya kidini na kujenga udugu na mapenzi miongoni mwa watu. Hata akasema kuwa mkutano huu usichukuliwe kama mikusanyiko mingine ya kawaida bali Allah mwenyewe huleta shani yake na msaada wake. Ili kufanikisha mkutano huu iwe katika ngazi ya kimataifa, kitaifa au hata kimkoa mara nyingi huundwa kamati mbalimbali kwa lengo la kuharakisha utekelezaji wa majukumu kwa ufanisi kwa njia iliyo bora. Sambamba na hilo, katika Mkutano wa Mwaka wa 48 wa Jumuiya ya Waislamu Waahmadiyya Tanzania ziliundwa kamati au idara mbalimbali. Miongoni mwa idara hizo ni idara ya Vyombo vya Habari na televisheni ya MTA.

Idara ya habari ilipewa majukumu kadhaa ikiwa ni pamoja na kuhakikisha kuwa habari za Jalsa Salana zinatangazwa vyema kwenye vyombo vya habari ambapo wajumbe wake walijitahidi kuhakikisha kuwa azma hiyo inatia.

Kwa msaada wa Allah, ilishuhudiwa vyombo vya habari vya redio, televisheni na magazeti na hata kupitia mitandao ya kompyuta

Endelea uk. 2



Waziri Mkuu akiwahutubia waumini wa Jumuiya ya Waislamu Waahmadiyya katika Mkutano wa Mwaka wa 48 uliofanyika katika eneo la Kitonga, Manispaa ya Ilala, Dar es Salaam.

Mapenzi ya Mungu
Maoni ya Mhariri

KARIBU 2018

Ni vigumu, na kwa hakika haiwezekani kuzihesabu neema za Allah Alizotupa sisi binadamu. Tizama kwa jicho la yakini. Limeumbwa jua ili litutumikie sisi na vitu vyote vimeumbwa virahisishe safari ya binadamu ili kumuabudu Muumbaji wa mbingu na ardhi. Mengine yote hayana uzito kuliko kumuabudu Allah na kumtegemea.

Ni masikitiko makubwa ya kwamba tunatumia muda mwingi kuyafanya yale yaliyotakiwa kuwa ya mwisho kuwa ya kwanza. Aghalabu tunaacha kabisa lile jambo la msingi na kama alivyowahi kusema mshairi wakandikaje kwa nje penye mwanya hupaoni.

Tunamshukuru sana Allah kutupa nguvu na afya ya kuingia katika mwaka mpya 2018. Wakati tunaingia katika mwaka mpya, inatubidi tukumbushane. Sala ni chakula cha roho. Ukikosa utakonda na hatimaye kudhoofika. Ni chakula kinachotakiwa kuliwa mara tano kwa siku. Na wakati dunia ipo kimya usiku unaamka kumshukuru Allah. Hiyo ndiyo njia pekee ya kukabiliana na madhila na maumivu yanayotukabili hivi leo. Mahangaiko yamezidi. Wasiwasi umetanda kila mahali. Vita na uhasama vimeifunika dunia. Ni wapi pa kukimbilia kama si kwa Allah?

Wewe unadhani mashaka aliyoyakabili Mtukufu Mtume Muhammad s.a.w angeyawezaje bila silaha ya sala. Mipango ilifanywa ya kumdhuru akatoka Makka, akaingia pango la Thaur na kufika Madina salama salimini. Siri yake ni nini kama sio sala za vilio machozi kutiririka.

Maadui hawakumuacha. Walimfuata hadi Madina na akalazimika kulinda uhuru wa kuabudu. Watu 313 dhaifu, wasio na silaha, wasio na uzoefu wa vita wakawachakaza mahodari wa vita. Siri yake ni nini? Sala za vilio.

Watu wa Uarabuni walikuwa wameharibik mno, ulevi na madhambi mengine makubwa, hata uturi wote wa Uarabuni usingeweza kuondoa uvundo uliokuwa umetapakaa. Masihi Aliyeahidiwa Hadhrat Mirza Ghulam Ahmad a.s. anaeleza vizuri hali yao:

Uliwakuta vinyesi, kwa kuzingwa na maasi,

Lakini kwa sala za vilio:

Akawafanya fususi, za dhahabu za thamani.

Mtume Muhammad (s.a.w.) akawafanya Waarabu fususi – siri yake ni nini? Sala za vilio.
Kumbe dawa ya matatizo yetu tunayosala. Tusimamishe sala na katu tusichoke kumsalia Mtukufu Mtume Muhammad (s.a.w.). Ukiwa shambani. Ukiwa kwenye basi. Chochote unachokifanya unao wakati mzuri wa umsalia mtukufu Mtume Muhammad (s.a.w.)

Kwa silaha hizi mbili, InshaAllah tutafanikiwa kupata shabaha ya kuumbwa kwetu na huo ndio ufaulu mkuu.

Binadamu kama anavyosisitiza Allah katika Quran tukufu, ni dhaifu tena ni dhaifu sana, dawa mjarabati ni kukumbushana mara kwa mara kuhusu silaha hizi mbili na kwa hakika kukumbushana kunafaa.

Shani ya Jalsa Salana 2017 kupitia vyombo vya habari

Kutoka uk. 1

vikitangaza habari za mkutano siku chache kabla ya mkutano na pia siku za mkutano. Vyombo hivyo vilitia fora siku ya Jumapili ya tarehe 1 Oktoba, 2017 wakati Mgeni Maalum, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania alipofika kushiriki Mkutano. Taarifa za habari za redio na televisheni jioni hiyo zilipambwa na kuongoza kwa habari za mkutano wa mwaka wa Jumuiya ya Waislamu Waahmadiyya Tanzania achilia mbali magazeti mengi ya siku iliyofuata ya tarehe 2 Oktoba, 2017 ambapo habari za Jalsa ziligonga vichwa vya habari vya magazeti hayo tena katika kurasa za mbele. Kwa kutaja machache, gazeti la "*Daily News*" linalomilikiwa na Serikali liliandika "***Peace Security in your hands***". Nalo "*Habari Leo*" ambalo pia linamilikiwa na Serikali liliandika "***Viongozi wa kidini wapewa maagizo mazito ya kiusalama***". Gazeti la "*Nipashe*" liliandika "Majaliwa ataja dawa wavurugaji". Kwa upande wake, "T*anzania Daima*" lilijinadi "***Majaliwa: Wapigeni vita wanaotaka kuvuruga Amani***". "*Uhuru*" nalo halikubaki nyuma kwani katika ukurasa wake wa mbele liliongozwa na habari "***Majaliwa aagiza wanaovuruga Amani wafichuliwe***". Kama hiyo haitoshi gazeti la *Habari leo* katika ukurasa wake wa mbele lilipambwa na picha ya Waziri Mkuu akipokea zawadi ya kitabu kutoka kwa katibu wa malezi wa Jumuiya ya Waislamu Waahmadiyya Tanzania, Mahmood Hamsin Mubiru huku kulia akionekana Amir na Mbashiri Mkuu Sheikh Tahir Mahmood Chaudhry.

Gazeti la *Mtanzania* lilitoa picha inayoonesha Waziri Mkuu akizungumza na waumini wa Jumuiya ya Waislamu Waahmadiyya.

Msaada wa Allah

Kwa msaada wa Allah, uwepo wa Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa ambaye alikuwa Mgeni Maalum siku ya kufunga mkutano, uliongeza hamasa ya kutangazwa kwa habari ya Mkutano kwenye vyombo vingi vya habari kwani alivitaka vyombo hivyo bila kukosa viripoti tukio la Mkutano. "Nimefurahi kuwa vipo vyombo vya habari hapa, hivyo naagiza kwamba hotuba hii isambazwe kwenye vyombo vingine vyote vya habari ili viweze kutoa habari za mkutano huu, alisisitiza.

Kama alivyoagiza Waziri Mkuu, kwa masaada wa Allah jambo hili lilitekelezwa barabara. Ilishuhudiwa vyombo vya habari vya redio na televisheni kuanzia jioni hadi usiku vikiwemo *Redio Clouds FM*, *Redio One*, *TBC Taifa*, *ITV*, *Channel Ten*, *TBC1*, *Azam TV* (kwa kutaja vichache tu) vilitoa habari za Jalsa kwenye Taarifa za Habari ambazo husikilizwa na watu wengi zaidi hasa nyakati za jioni na usiku. Habari hizo zilipewa umuhimu wa mwanzo kabisa kwenye taarifa za habari za redio na televisheni. Kama vile hiyo haitoshi, matoleo ya magazeti ya siku iliyofuata (Jumatatu tarehe 2 Oktoba, 2017) ya Kiswahili na Kiingereza na yanayosomwa kwa wingi yaliripoti habari za Jalsa tena katika kurasa za mbele, huku mengi yakimkariri Waziri Mkuu aliyehamasisha suala la umuhimu wa taasisi na madhehebu ya dini kuhubiri Amani ya nchi. Ujumbe huo wa Waziri Mkuu kwa hakika uliendana na kaulimbiu ya mkutano wa mwaka huu isemayo "Muislamu wa kweli ni yule ambaye watu wengine wote wako salama dhidi ya shari ya ulimi wake na mikono yake."

Magazeti yaliyotoa habari za Jalsa siku ya Jumatatu tarehe 2 Oktoba, 2017 ni pamoja na magazeti ya kiingereza *Daily News* na *Citizen*, magazeti ya Kiswahili *Nipashe*, *Uhuru*, *Tanzania Daima*, *Mtanzania*, *Mwananchi* na *Habari Leo*.

Ingawa siku Waziri Mkuu alipohudhuria kwenye Jalsa vilikuwepo vyombo vya habari vichache vilivyofika kuripoti habari za Jalsa, lakini baadaye asilimia kubwa ya vyombo vya habari viliripoti habari za Jamaat kama tulivyoona.

Tukio hili kwa namna moja au nyingine naweza kulifananisha na tukio lililoripotiwa na Bwana Abid Khan kuhusu baadhi ya vyombo vya habari wakati Kiongozi Mkuu wa Jumuiya ya Waislamu Waahmadiyya Duniani, Hadhrat Mirza Masroor Ahmad a.t.b.a alipozuru Canada mnamo Oktoba-Novemba, 2016. Akiripoti tukio hilo, alisema kuwa vyombo vingi vya habari nchini Canada vilihudhuria na kuripoti kwa shauku habari za Jalsa. Hata hivyo, gazeti moja la Serikali (*The Globe and Mail*) lilikataa. Inasemekana gazeti hilo lilihitaji kusikia habari kutoka kwa kiongozi wa waislamu ambaye anahamasisha Amani na uvumilivu lakini mara ilipopatikana fursa ya kusikiliza ujumbe wa Khalifatul Masih wakaiacha bila kuiripoti. Inaelezwa kuwa katika juma hilohilo la Jalsa gazeti likaamua kwenda kutoa habari kuhusu wakimbizi wa Syria ambapo waandishi wa gazeti hilo waliwauliza wakimbizi hao kuwa watakuwa wakishughulika na nini mwishoni mwa juma. Kwa bahati waandishi hao ikatokea wakawasiliana na baadhi ya wakimbizi wa Kiahmadiyya. Kwa hakika haikuwa bahati bali ilikuwa mipango ya Allah, wakimbizi hao walisema kuwa watatumia siku zao za mwishoni mwa juma kushiriki katika Jalsa Salana ya Canada na hivyo wakamwalika mwandishi huyo aungane nao kushiriki Jalsa Salana hiyo. Hivyo, mwandishi Patrick Collins alihudhuria Jalsa na aliandika makala ambayo ilieleza kwa kina kuhusu Jalsa Salana ambapo pia kwenye makala hayo alitoa picha ya Khalifa Mtukufu a.t.b.a. Aidha, aliandika kuwa wakimbizi wa Syria wanashukuru kuwa wameweza kukimbia nchi yao yenye vita na kuja kukutana na Imamu wao mpendwa kwenye Jalsa Salana. Gazeti hilo hilo ambalo halikupenda kuandika habari za Jalsa likajikuta likiishia kuandika moja ya makala si tu nzuri na ndefu bali yenye kuvutia. Akielezea tukio hilo, Khalifa Mtukufu a.t.b.a alionyesha kufurahishwa na akasema kuwa ndio jinsi Allah Anavyoisaidia Jamaat.

BODI YA UHARIRI

Msimamizi: Sheikh Tahir M. Chaudhry - Amir Jamaat, Tanzania.
Mhariri: Mahmood Hamsin Mubiru.
Kompyuta: Sheikh Abdulrahman M. Ame.
Mchapishaji: Sheikh Bashart Ur Rehman
Msambazaji: Mwl. Omar Ali Mnungu
Wajumbe:
1. Mwl. Abdullah Khamis Mbanga
2. Dr. Swaleh Kitabu Pazi
3. Jamil Mwanga.
4. Abdillah Kombo

Makao Makuu - Ahmadiyya Muslim Jamaat Tanzania,
Mtaa wa Bibi Titi Mohammed, S.L.P. 376.
Simu 022 - 2110473, Fax 022 - 2121744, Dar es Salaam, Tanzania.
Email: mapenziyamungu36@gmail.com

Mtume s.a.w. ni Rehema kwa Ulimwengu

Kutoka uk. 1

Waahmadiyya na huwavurumishia matusi kwa jina la mpendwa wetu Mtukufu s.a.w. na hii hufanywa kila siku lakini kwa kusheherekea siku hii, mathalani hata hii leo imeongezeka zaidi. Kwa kufanya hivyo wanadhani ndio wananyanyua heshima na Utukufu wa Mtume huyu adhimu. Vizuizi vimewekwa kuzuia shughuli za kila siku na hakuna uwezekano wa kwenda shuleni, hospitalini na madukani na kwa kuongezea tu mamilioni ya pesa hupotea katika uchumi, na yote haya eti ni kwa kumpenda Mtukufu Mtume s.a.w, ambaye alishawaambia wafuasi wake kuwa kwanza epukeni kukaa mitaani na kama ni lazima basi epukeni kusababisha huzuni, sambazeni amani, inamisheni macho yao, na fanyeni matendo mazuri na wazuieni wengine kufanya maovu.

Lakini hawa wanaojitangaza kwa shangwe kuwa wasimamizi wa dini hudhani wanawajibu wa kumwita yeyote kafiri au muaminio kulingana na matakwa yao binafsi. Hakuna kitu kama hicho kulingana na mafundisho na mfano wa Mtukufu Mtume s.a.w. Watu hawa wanaweza kuendelea kufanya watakavyo, lakini sisi Waahmadiyya tunalazimika kufuata kila muelekeo wa mfano wa Mtukufu Mtume s.a.w.

Hudhur alitaja baadhi ya vipengele vya mfano mwema wa Mtukufu Mtume s.a.w.

Masihi Aliyeahidiwa a.s. anasema kuhusu Mtukufu Mtume s.a.w kumpenda Allah ambapo Mtukufu Mtume s.a.w. alikuwa na mapenzi makubwa mno na Allah kiasi hichi kwamba watu walisema Muhammad s.a.w. amelevywa na mapenzi ya Mola wake.

Kisha, katika kutaja Mapenzi ya Mtukufu Mtume s.a.w. kwa Allah Mtukuka, Masihi Aliyeahidiwa a.s. aliandika kwamba wakati aya kuwahusu waabudu masanamu kuwa najisi, wachafu na kizazi cha Shetani ziliposhushwa, Abu Talib alimuonya Mtume s.a.w. juu ya matokeo ya kutisha. Mtukufu Mtume s.a.w. alisema kuwa hatajali kama atapoteza maisha yake kutokana na ujumbe wake na alimtoa hofu Abu Talib kuwa angeweza kuondoa ahadi yake ya kumlinda. Lakini Abu Talib alishangaa sana kwa uimara wake huo ambapo alimuhakikishia kumpatia msaada wake maadamu akiwa hai.

Jinsi Masihi Aliyeahidiwa a.s. alivyofafanua tukio hilo hapo juu, ameonesha mapenzi yake kwa Mtukufu Mtume s.a.w. Masihi Aliyeahidiwa a.s. zaidi ya hapo akaeleza, siku zote naangalia kwa mastaajabu juu ya cheo cha juu cha Mtume huyu wa Uarabuni, Muhammad s.a.w, naomba maelfu ya rehema na amani ziwe juu yake. Ni vigumu kutathmini upeo wa juu wa cheo chake na haiwezekani kwa mtu kutathmini nguvu yake ya kiroho. Ni bahati mbaya kwamba cheo chake hakijatambuliwa kama ilivyopasa. Ni yeye aliyefanikiwa sana kuurejesha tena umoja wa Mungu, ambao ulifutika kabisa katika ulimwengu. Alimpenda sana Mungu kwa viwango vya juu kabisa na roho yake ilizama kabisa katika kuonesha huruma kwa wanadamu. Hivyo basi, Mungu aliyetambua siri za moyo wake, alimpatia ubora juu ya Manabii wote na kwa kila mtu, aidha waliopita au wajao. Alimpatia matamanio yake katika maisha yake.

Ni chemchem ya baraka zote. Yeyote anayedai kupata ubora wowote bila ya kufaidika na yeye huyo si mwanadamu, bali ni kizazi cha shetani, ufunguo wa kila ustawi ulikabidhiwa kwa Mtukufu Mtume s.a.w. na amepewa kila hazina ya ufahamu (wa Mungu Mwenyezi). Kama mtu atakataa fursa ya kufaidika naye, basi atanyimwa milele.

Sisi ni kina nani na tuna umuhimu gani? Naweza kuhesabika kuwa mkosefu wa shukurani kama sitakiri kuwa nimepata umoja wa kweli na kumtambua Mungu aliye hai kupitia mwanga wa Mtume huyu s.a.w. Tumekuwa na heshima ya kupokea ufunuo na kuanzisha mazungumzo na Mungu na kwa njia hii tuliweza kukutana naye.

Kiini cha madai ya Masihi Aliyeahidiwa a.s. ni kuwa ukaribu na Allah unaweza kupatikana tu kwa kumfuata Mtukufu Mtume s.a.w. katika mfano wake wa ibada kwa kuzingatia umakini na kujitolea. Kwa mujibu wa hadithi moja, sahaba ambaye alishuhudia Mtukufu Mtume s.a.w. akifanya ibada ya nafal akiwa faraghani, anasema kwamba aliweza kusikia sauti kutoka kwenye kifua cha Mtume Mtukufu s.a.w. ambayo ilikuwa sawa na sauti zinazozalishwa kutoka kwenye mawe yanayosigana kwa kuzalisha unga wa nafaka.

Wakati fulani Hadhrat Aisha r.a. alimuuliza Mtume s.a.w. sababu ya kubeba usumbufu wote huo ambapo dhambi zake za zamani na za baadaye zilishasamehewa, alijibu kwa kusema 'Je, silazimiki kuwa mtumishi mwenye shukrani kwa Mungu Mwenyezi? Masihi Aliyeahidiwa a.s anasema kwamba Mtukufu Mtume s.a.w alileta mabadiliko katika maisha ya Waarabu kutoka kwenye hali ya kuwa kama wanyama na kufikia kiwango cha juu sana kwamba walitumia usiku wao kwa kuabudu.

Ni wajibu wetu kuishi kulingana na viwango hivyo. Hudhur alisema kuwa ripoti kutoka kwa Tanzimu na Jamaat inasema kwamba asilimia kadha wa kadha hushiriki katika sala, lakini kama haijakuwa asilimia 100%, hatuwezi kupata utulivu. Ni juu ya mtu binafsi na wajibu wa Jamaat kuboresha hali hii.

Ukweli wake (Mtukufu Mtume s.a.w.) ulikuwa ni wa kiwango cha juu sana kiasi kwamba mmoja wa maadui wake wabaya sana alishuhudia, akielezea mifano kutoka hatua zote za maisha. Pia, Abu Jahl hakuwa na uwezo wa kukataa kwamba Mtukufu Mtume s.a.w. daima alikuwa mkweli. Abu Sufyan pia alisema katika mahakama ya Heraclius kuwa Mtukufu Mtume s.a.w. hakuwahi kuongopa. Msomi wa Kiyahudi ambaye alimwona Mtume s.a.w pia alisema kuwa huu sio uso wa mwongo.

Hata leo hii, ukweli wa mafundisho na matendo yake yanaweza kuwaleta wasio Waislamu karibu na Uislamu, tofauti na uongo, ubunifu na udanganyifu. Waahmadiyya lazima daima kujitahidi kuongeza kiwango cha ukweli kwa kufuata mfano wa Mtume s.a.w. Ikiwa hakuna ukweli katika vitendo vya mtu basi watu pia watachukua mafundisho ya kidini kama uongo. Kuwepo kwa Mungu na dini ya Uislam ni ukweli. Ni wajibu wetu kueneza ukweli huu kwa njia ya ukweli.

Masihi Aliyeahidiwa (as) anasema kwamba wakati Mtume Mtukufu (saw) anatokea, dini zote za nyuma zilikuwa zimepoteza Ucha Mungu. Aliurudisha Umoja wa Mungu kwenye dunia hii na akaleta mapinduzi katika maisha ya watu kiasi kwamba wanyamapori wakageuzwa kuwa watu, kisha wakawa watu walioelimika na mwishowe wakawa watu wa Mungu.

Hivyo, ili tuwe Waislamu wa kweli na tujenge maungano na Mungu wa kweli, tunapaswa kuinua daraja la ukweli wetu. Ni Waahmadiyya pekee wanaoweza kufanya hivi kwani wameahidi kutoa kipaumbele kwa dini yao juu ya dunia. Kisije kikabakia kuwa kiapo kitupu tu, badala yake, matendo yetu yote ni lazima yatoe ushahidi kwa hilo.

Khulka za hali ya juu za Mtume Mtukufu (saw) ni pamoja na huruma na kutopenda makuu. Hadhrat Aisha (ra) anasimulia kwamba kila mara mtu yeyote alipokwenda nyumbani kwake daima alikuwa akimpokea vizuri. Hii ndio sababu Allah Anasema ndani ya Kuruani Tukufu: Kwa hakika una khulka njema, tukufu. (Al Qalam 5). Mtume Mtukufu (s.a.w.) alisema "Mimi ni Chifu wa uzao wa Adam, lakini sijivuni chochote na hilo. Katika Siku ya Hukumu bendera ya sifa itakuwa mikononi mwangu, lakini sijivuni chochote kwa hilo.

Masihi Aliyeahidiwa (as) anasema kwamba Mtume Mtukufu (saw) alikuwa ni mtu mkubwa kuliko wote lakini alikuwa mpole sana katika nyenendo zake kiasi kwamba mfano mmoja wa upole wake na kutopenda makuu unapatikana katika Kuruani Tukufu. Siku moja Mtume Mtukufu (saw) alijiwa na mtu mmoja kipofu wakati akiwa anazungumza na viongozi fulani wa Makka. Allah Taala Amefunua sura ya Kuruani Tukufu na Mtume Mtukufu (saw) akaenda nyumbani kwa mtu yule kipofu na akampa nguo yake. Masihi Aliyeahidiwa (as) anasema kwamba watu wanaomuelewa Mungu Mwenyezi daima wanakuwa wapole kwa sababu daima wanamukhofu Mungu. Kama ambavyo Anatoa zawadi kwa vitendo vyema vidogo sana. Pia anakerwa na madhambi madogo sana.

Hadhrat Aisha (ra) anasimulia kwamba mtu mmoja aliomba kumuona Mtume Mtukufu (saw). Mtume Mtukufu akamwambia Hadhrat Aisha (ra) kwamba alikuwa ni kaka mbaya na mtoto mbaya wa kiume. Alipokuja na kukaa Mtume Mtukufu (saw) akamkarimu sana. Alipoondoka, Hadhrat Aisha (ra) akamuuliza kwa nini alikuwa amemfanyia ukarimu kiasi kile ilhali alikuwa ni mtu mbaya. Mtume Mtukufu (saw) akasema kwamba yeye daima huwa mkarimu kwa watu na katika Siku ya Hukumu mtu mbaya kabisa atakuwa yule ambaye watu wanamkwepa kwa kukhofu shari zake. Siku moja Mtume Mtukufu (saw) aliulizwa ni jinsi gani ya kujua kama mtu ni mbaya au ni mwema, alisema kwamba kama jirani zako wanasema wewe ni mtu mwema, basi uwe na uhakika kwamba tabia yako ni nzuri.

Hivyo, ni wajibu kwa kila Muahmadiyya kuufuata mfano huu. Majanga mengi katika nchi za Kiislamu za leo yanatokana na kuporomoka kwa viwango vya imani zao na kusahau kwao mfano mwema wa Mtume Mtukufu (saw).

Masihi Aliyeahidiwa (as) pia anasema kwamba Mtume Mtukufu (saw) alikuwa ni mfano wa vitendo vyote vyema. Ni lazima tuone ni jinsi gani alivyowatendea wanawake. Mtume Mtukufu (saw) alikuwa ni mtu mstaarabu na mstahimilivu. Hata kama mwanamke mzee akimwambia abakie sehemu fulani, atabaki sehemu hiyo mpaka ampe ruhusa ya kuondoka. Siku moja alileta kitu na sahaba wake mmoja akaomba ampokee lakini alikataa akisema kwamba ni lazima ubebwe na mwenye mzigo wake. Mtume Mtukufu (saw) alipopitisha miaka 13 ya utume wake katika hali ya shida na miaka 10 akiwa katika mamlaka na ustawi. Miongoni mwa wapinzani wake walikuwa ni watu wake mwenyewe, Mayahudi, Wakristo, Washirikina, Wachawi na kadhalika. Walikuwa wakinywa kupita kiasi na wakiona vitu vilivyokatazwa kuwa ni halali. Kuua hakukua na maana zaidi ya kukata mbogamboga kwao.

Hali katika Makka ilikuwa ni mbaya sana kiasi kwamba waliteseka kwa njaa na kunyanyaswa na wafuasi wa Islam walikuwa wakipigwa kila siku. Kisha walifukuzwa kwenye mji wao wa nyumbani. Kisha wakati wa kipindi cha pili cha Mtume Mtukufu (saw) alitawala Arabia yote. Kama angekuwa mchoyo, angekuwa na fursa safi sana ya kufanya hivyo. Lakini alipoiteka Makka alieleza kwamba hakuna yeyote atakayepata lawama. Khulka za hali ya juu za Mtume Mtukufu kweli zilipata majaribu na akaonyesha subira, Ucha Mungu, upole, ushujaa na wema na kadhalika.

Hivyo sherehe za leo ni lazima zifanyike kwa kufuata mfano mwema wa Mtume Mtukufu (saw) kwa kuwa na viwango vya juu vya ibada, kujizamisha kabisa katika Tauhiid na khulka za hali ya juu. Kama hatufuati mfano huu, kutakuwa hakuna tofauti kati yetu na wengine ambao wamegawanyika kwa kuwafuata viongozi wao wa kidunia na hao wanaoitwa mashekhe. Kwetu sisi, hitajio la ahadi ya baiati kwa Masihi Aliyeahidiwa (as) ni kwamba matendo yetu yote yanafanyika kwa kuzingatia mfano wa Mtume Mtukufu (saw). Ninamuomba Allah Atuwezeshe sote kufanya hivyo, Amin.

Masihi Aliyeahidiwa (as) anasema "Mtu Yule ambaye alikuwa ni mkamilifu kupita wote na mtu asiyekuwa na kosa lolote na Mtume safi, ambaye ameleta Baraka kamili ambazo kwazo kulikuwa na uhuishaji wa kiroho na kukua na dhihirisho la kwanza la Siku ya Hukumu lilijionesha duniani. Na kwa kupitia yeye dunia nzima iliyokufa kiroho ikaja huika; Yule Nabii aliyebarikiwa alikuwa ni Muhuri wa Manabii, Kiongozi wa walio mukhlis, Muhuri wa Mitume na Fahari ya Manabii, Muhammad Mteule (saw). Ee Mungu Mpendwa! Teremsha Baraka Zako na Rehema kwa Mtume huyo Mpendwa ambazo haujaziteremsha kwa yeyote tokea mwanzo wa wakati. Kama Mtume huyu Mtukufu asingetokea duniani basi tusingekuwa na ushahidi wa ukweli wa manabii wa daraja za chini kama vile Yona, Jobu, Isa bin Maryam, Malakai, Yohana, Zakaria na wengineo, lakini walikuwa wamepewa ukaribu, heshima na walikuwa wapendwa wa Mungu. Ni wema wa Mtume huyu kwamba watu hawa wamekubalika kuwa wakweli. "Ee Allah Teremsha Baraka na Rehema Zako juu ya Mtume Mtukufu (saw) familia yake na masahaba zake. Wa aakhiru daawana anilhamdulillahi rabil aalamiin.

Hazur (atba) aliwataja marehemu wachache na kuongoza sala zao za jeneza ghaib. Kati yao wa kwanza alikuwa ni dada Salma Ghani aliyekuwa akiishi Philadelphia, Marekani, aliyefariki tarehe 20 Novemba akiwa na umri wa mika 83. Amir Sahib wa Jamaat ya Marekani anaandika kwamba alijaza Baiati na kujiunga na Jumuiya mwaka 1960 au 61 akiwa na umri wa miaka 24. Kazi yake alikuwa ni mwalimu. Mwaka 1975/76 alihudhuria Jalsa huko Rabwah ambapo alikutana na Hadhrat Khalifatul Masih III (rh). Alikuwa ni Sadr Lajna kwa miaka 15 kwa juhudi kubwa na aliipaisha Lajna Imaillah kwenye ngazi mpya kabisa. Pia alikuwa ni Sadr Lajna wa Jamaat ya Philadelphia katika nyakati tofauti nyingi. Ukiacha

Endelea uk. 4

Tunalo Somo katika Maisha ya Mzee Sultan Ungando

Na Al –Ustadhi Khamisi Wamwera – Dar es salaam

Sultani Mohammed Ungando si jina geni sikioni mwa wanajumuiyya wengi nchini Tanzania. Anafahamika ni mzee aliyejitolea sana katika Ahmadiyya. Alikuwa Mwanajumuiyya aliye mstari wa mbele kujitolea katika shughuli mbalimbali za Jamaat. Kwa njia hii alitambulika sehemu kubwa ya nchi yetu.

Hivi sasa mzee huyu ni marhumu. Ijumaa ya tarehe 08/12/2017 mnamo saa 3:00 usiku, aliaga dunia. Binafsi naweza kusema ni miongoni mwa misiba adhimu. Kwa hakika sisi ni wa Allah na Kwake ndiko marejeo yetu. Hapana shaka kifo pia ni rehema ya Mwenyezi Mungu.

Kwa wale wasiomtambua mzee Sultani Ungando ndio hapa chini nitaeleza khabari zake ijapokuwa kwa uchache sana ili kupata taswira sawasawa. Mzee Sultani Mohammed Ungando alizaliwa katika kitongoji cha Kipale, tarafa ya Muhoro wilaya ya Rufiji mnamo mwaka 1924. Yeye ni mtoto wa tatu katika wanaume. Wazazi wake walikuwa wakulima. Kwa kushughulika na kazi hii, babaye alikuwa mtu maarufu sana. Nyumba yao haikuwa tupu, bali kila wakati walikuwa na neema ya vyakula mbalimmbali. Mpunga, mahindi, kunde, mbaazi na minazi. Pamoja na hayo mnamo mwaka 1936 Sultani Ungando na familia yake walihamia kijiji cha Mbuchi ambako walianza maisha mapya. Mwaka 1939 Mzee Ungando akiwa na umri wa miaka 15 baba yake alifariki. La kupendeza ni kwamba kabla Mzee huyo hajaaga dunia, Mzee Sultani Ungando tayari alikwisha pelekwa chuoni. Naam hivi ndivyo ilivyokuwa. Baada ya baba yake kufariki, Mzee Sultani Ungando alilelewa na Bwana Athumani Shamte Malumbwa. Lakini baada ya mamaye kuolewa na mume mwingine, Mzee Ungando ikabidi amfuate mama yake. Hiyo ilikuwa mnamo mwaka 1940 wakati Bw. Athumani Mohammed Mlekelwa Mpogo alipomzawiji Bimkubwa huyo.

Mzee Sultani Ungando aliendelea na masomo ya chuo kule Kiongoroni kwa Mwalimu Jabir Adam ambako alikutana na Mzee Aliy Salum Ndendekele ambaye naye hivi sasa ni marehemu. Huko wakawa pamoja katika kutafuta elimu. Kumbe! Uswahiba wao ulianzia mbali.

ANAPELEKWA SKULI.

Mwaka 1944, Mzee Sultani Mohammed Ungando alipelekwa shule. Akiwa na umri wa miaka 20, alianza masomo ya shule pale Muhoro Primary School. Kwa wakati ule watoto waliingizwa na kuanzishwa masomo ya skuli wakiwa na umri mkubwa. Hata hivyo, waalimu wa shule hiyo hawakumwanzisha darasa la kwanza baada ya kuona uwezo wake. Mzee Ungando kabla alikuwa na uwezo wa kusoma, kuandika na kuhesabu. Kwa hali hiyo waalimu walimwanzisha darasa la pili. Siku za kwanza alikuwa anatoka kitongoji cha Kipale hadi Muhoro. Umbali wa mwendo wa masaa mawili na nusu hivi. Lakini badaye hali ilibadilika. Mipango ikapangwa na sasa ikabidi Mzee Ungando aishi pale pale Muhoro kwa babu yake mdogo Mwalimu Rashidi Mussa Ungando. Lakini Mzee Sultani Ungando hajakaa muda mrefu babu yake mwalimu Rashidi Mussa Ungando alipewa uhamisho wa kwenda Kibiti. Kwa hiyo Mzee Sultani akaendelea na ile safari yake ya kutoka Kipale hadi Muhoro kwa masomo. Mwaka 1946 shule ya Kibiti ilifungwa kwa sababu ya njaa kali iliyotokea. Warufiji wenyewe njaa hiyo waliipachika jina la "Njaa ya John Young". John Young alikuwa D.C wa serikali ya Kiingereza wakati huo. Kwa hiyo Mwalimu Rashidi Mussa Ungando hakukaa sana Kibiti akahamishiwa Mafia. Wakati huo Mafia na Rufiji ilikuwa wilaya moja.



Mzee Sultani Mohammed Ungando, kwenye siku za mwishoni mwa uhai wake

Mzee Sultani Ungando aliendelea vyema na masomo yake pale Muhoro. Mungu bariki, mnamo mwaka 1947 alifaulu mtihani wake wa darasa la nne na kuingia shule ya Utete Middle School ambako hadi mwaka 1950 alihitimu darasa la nane. Mwaka uliofuata, yaani mwaka 1951 Mzee Sultani Ungando alijiunga na shule ya ufundi kule Ifunda – Iringa. Alikuwa kule hadi mwishoni mwa mwaka 1953. Mwaka 1954 hadi mwishoni mwa mwaka 1955 alikuwa Lindi katika mazowezi ya mafunzo ya kazi. Mwaka 1956 Mzee Sultani Ungando alimaliza na kuhitimu mafunzo hayo ya ufundi wa magari.

ANAAJIRIWA TOM GARAGE.

Maisha ya shule yameisha, sasa Mzee Sultani Ungando anaanza maisha mapya ya kujitegemea. Kwa kuwa alikuwa na ujuzi wa magari, basi hakusumbuka sana. Akaajiriwa kwenye Karakana ya 'Tom Garage' kwa mshahara wa shilingi 100. Kwa wakati ule, hii ilikuwa kampuni na gereji kubwa. Hata hivyo, Mzee Ungando alikuwa pale kwa muda mfupi sana. Alifanya kazi hapo kwa kipindi cha miezi sita tu kisha akaacha kazi. Aliacha kazi kwa sababu aliona mshahara ni mdogo. Haya yalikuwa kule Lindi baada tu kumaliza mafunzo yake ya ufundi.

Baada ya hapo alirejea kwanza Rufiji kwa siku chache halafu akaja hapa Dar es salaam. Kulikuwa na kampuni moja kubwa sana ikiitwa '*Cooper Motor Company Limited*'. Ilikuwa inashughulika na magari. Kutengeneza kwa kuyakarabati na kuuza magari mapya. Basi Mzee Ungando mara mbili alikwenda kwenye Ofisi hiyo kwa kutaka kufanya kazi huko. Alionesha vyeti vyake vinavyoeleza ujuzi wake wa magari. Meneja Uajiri akiwa Mzungu alimwambia Mzee Ungando kuwa kufuatana na vyeti vyake alivyonavyo, kampuni yao ilikuwa haina nafasi ya kumwajiri. Hata hivyo Mzee Ungando alifika tena kwa mara ya tatu na kuiambia Ofisi imwajiri kwenye nafasi yoyote iwayo. Basi yule Mzungu Meneja Mwajiri akamwajiri Mzee Ungando kwa mshahara wa shilingi 200 kwa mwezi.

Jina la Mzee Ungando lilipelekwa kwa Bw. Fedha ambaye alikuwa Mhindi. Ilikuwa ni nakala ya barua aliyoandikiwa Mzee Ungando inayoeleza tangu siku ile ameajiriwa na kampuni hiyo na mshahara wake utakuwa kiasi hicho. Bwana fedha huyo wa kampuni aliona huo ni mshahara mkubwa sana, Mzee Sultani hakustahili kuupata. Yeye kwa mdomo alimueleza Mzee Ungando kuwa atapewa mshahara wa shilingi 100 kwa mwezi. Mzee Ungando hakutaka kufanya kama kule Lindi wa kunyuruka, bali alikubaliana na bwana fedha huyo. Siku ileile akaanza kazi. Ya Allah ni mengi, Humsaidia mja wake wakati wowote na khasa yule anayedhulumiwa. Kwa miezi michache sana kupita, kampuni iliridhika mno na utendaji kazi wa Mzee Ungando. Ghafla mshahara wake ulipanda kutoka hizo shilingi 100 hadi shilingi 300 kwa mwezi.

Mnamo mwaka 1956 chama cha wafanyakazi Tanganyika TFL chini ya uongozi wa katibu Mkuu wake Mheshimiwa Bw. Rashidi Mfaume Kawawa, kiliitisha mgomo wa wafanya kazi wote wa nchi nzima. Ilitakiwa wafanyakazi wote washiriki katika zoezi hilo. Wafanya kazi wote waafrika waliokuwa 'Cooper Motor Company Limited' walishiriki isipokuwa Mzee Sultani Mohammed Ungando na Wakenya wawili ambao hawakushiriki kwenye mgomo huo. Naam baadae kidogo walifika hapo viongozi wa TFL kuwauliza wale ambao hawakuunga mkono mgomo huo na kwa nini waliendelea kufanya kazi! Katika hawa watatu, kila mmoja alijieleza bila kuonekana na kosa au khatiya yoyote. Mzee Sultani Ungando aliendelea kupanda ngazi kila nafasi inapopatikana. Aliheshimiwa na kuaminiwa sana kule kazini kwake. Alistaafu mwaka 1990 baada ya kuitumikia '*Cooper Motor Company Limited*' miaka 35. Huu ni upande wa kimwili na dunia. Lakini sasa tuangalie upande wake wa kiroho na dini.

Tangu utoto na ujana wake, Mzee Ungando alikuwa karibu sana na mafundisho ya dini ya Kiislamu. Alikuwa mtu wa ibada mbalimbali. Pale alipokuwa mfanya kazi, hakuacha kutoa michango yake katika njia ya Mwenyezi Mungu. Alipolima mazao aliyokuwa anapata hakuyafanyia ubakhili, bali aliyatolea zaka na swadaka. Alikuwa anapenda sana kusoma vitabu mbalimbali khususan vya dini. Hakuwa mwenye papara na hasira ya karibu. Mkarimu tena alikuwa mwenye taadhima na heshima. Huendi kwake ukarudi patupu, labda awe hana chochote nyumbani mwake.

Endelea uk. 9

Mtume s.a.w. ni Rehema kwa Ulimwengu

Kutoka uk. 3

sala tano za kila siku, alikuwa haachi sala za Tahajjud. Alikuwa na hamu kubwa ya kwamba ujenzi wa msikiti umalizike huko Philadelphia na alikuwa akiombea hilo mara nyingi. Hivi karibuni utamalizika InshaAllah. Kwa maelezo ya raisi wa jamaat ya hapo alikuwa akionyesha utii kamili na ushirikiano kwa Jamaat ya hapo. Alipatikana na kansa ya tumbo miezi miwili iliyopita. Alimwambia wosia wake akisema kwamba kutokana na maelezo ya madaktari alikuwa na miezi mine mpaka sita ya kuishi, lakini anajua na siku chache tu zilizobaki. Aliacha maagizo kuhusu sala yake ya mazishi na kaburi ambalo tayari lilikuwa limeandaliwa.

Hakuwa na mtoto yeyote wala Muislamu mwingine yoyote katika familia yake lakini alikuwa na uhusiano mzuri sana na ndugu zake na wanafamilia wengine. Sadr Lajna wa Marekani anaandika kwamba malezi yake yalifanyika katika mazingira ya Kikristo, lakini alianza kuhoji imani za Kikristo akiwa na umri mdogo. Alisomea Ukatoliki, na pia dini zingine kama vile Ubudha, Uhindu na pia madhehebu zingine za Ukristo. Mmoja kati ya marafiki zake alimpa kipeperushi kwamba Mtume Isa (as) hakufa msalabani. Kilikuwa na majibu ya maswali yake yote. Kisha akaenda msikiti fulani na akanunua vitabu kadhaa. Alivisoma hivyo vitabu na kisha akajaza Baiati huko Philadelphia ambako aliishi hadi kifo chake.

Ameishi miaka 54 ya maisha yake kama Muahmadiyya, akionyesha viwango vikubwa vya upendo, mahaba na uyenyekevu kwa Jumuiya ya Ahmadiyya na Ukhalifa wa Ahmadiyya. Wakati wa zama za Hadhrat Khalifatul Masih IV (rh) alifanya kazi kama Sadr Lajna kwa miaka kumi na tano, baada ya hiyo pia alifanya kazi kama Mjumbe wa heshima wa Lajna Imaillah. Pia alifanya kazi kama kiongozi wa kamati ya ushauri ya Lajna kwa dawati la Afrika, na pia dawati la Amerika.

Daima alijikita katika kueneza ujumbe wa Islam. Kutokana na asili yake ya Kikristo alikuwa akieneza ujumbe kwa Wakristo kwa namna ya kisomi. Watu wengi waliikubali Ahmadiyya kutokana na juhudi zake, na hivyo akawa chanzo cha muongozo kwa watu wengi. Baada ya kutembelea kwa mara kadhaa huko Ghana na Nigeria, akawa anajulikana kama Auntie Salma Ghani. Daima atakumbukwa huko Marekani kwa Ucha Mungu wake na pia umaarufu wake.

Ninamuomba Allah Mwenyezi Ainue cheo cha marehemu na Awape uimara wale walioikubali Ahmadiyyat kutokana na yeye. Ninamuomba Allah Aiwezeshe Jamaat ya Marekani na watu wa Marekani kwa ujumla, kusikiliza na kukubali ujumbe wa kweli wa Islamu. Amin.

لَا إِلٰهَ إِلَّا اللّٰهُ مُحَمَّدٌ رَّسُولُ اللّٰهِ

AHMADIYYA MUSLIM JAMAAT TANZANIA CALENDAR

P. O. Box 376 Mnazimmoja, Dar es Salaam. Tel: +255 22 2111031, Fax: +255 22 2121744.
WEBSITES: www.alislam.org | www.ahmadiyyatz.org EMAIL: ahmusjamtaz@gmail.com



WAZIRI MKUU AKIWA KWENYE MAONYESHO YA VITABU WAKATI WA JALSA SALANA 2017



KHALIFA MTUKUFU WA V
HADHRAT MIRZA MASROOR AHMAD (atba)



MUONEKANO MPYA WA MAKAO MAKUU TANZANIA



AMIR NA MBASHIRI MKUU PAMOJA NA WAZIRI MKUU NA WANAJUMUIYYA KWENYE JALSA SALANA 2017

2018

2018 AD
1439 - 1440 AH
1397 HS



UFUNGUZI REDIO AHMADIYYA - MTWARA

January		Sulhu		Raby'al-Thaany - Jumaada al-awal		
Mon	Tue	Wed	Thu	Fri	Sat	Sun
1	2	3	4	5	6	7
8	9	10	11	12	13	14
15	16	17	18	19	20	21
22	23	24	25	26	27	28
29	30	31				

February		Tabligh		Jumaada al-awal - Jumaada al-Thaany		
Mon	Tue	Wed	Thu	Fri	Sat	Sun
			1	2	3	4
5	6	7	8	9	10	11
12	13	14	15	16	17	18
19	20	21	22	23	24	25
26	27	28				

20 - Siku ya Mwana Aliyeahidiwa

March		Amman		Jumaada al-Thaany - Rajab		
Mon	Tue	Wed	Thu	Fri	Sat	Sun
			1	2	3	4
5	6	7	8	9	10	11
12	13	14	15	16	17	18
19	20	21	22	23	24	25
26	27	28	29	30	31	

23 - Siku ya Masihi Aliyeahidiwa

April		Shahadat		Rajab - Sha'baan		
Mon	Tue	Wed	Thu	Fri	Sat	Sun
30						1
2	3	4	5	6	7	8
9	10	11	12	13	14	15
16	17	18	19	20	21	22
23	24	25	26	27	28	29

28 - 29 Shura ya Kitaifa

May		Hijrat		Sha'baan - Ramadhaan		
Mon	Tue	Wed	Thu	Fri	Sat	Sun
	1	2	3	4	5	6
7	8	9	10	11	12	13
14	15	16	17	18	19	20
21	22	23	24	25	26	27
28	29	30	31			

27 - Siku ya Ukhalifa

June		Ihsan		Ramadhaan - Shawwal		
Mon	Tue	Wed	Thu	Fri	Sat	Sun
				1	2	3
4	5	6	7	8	9	10
11	12	13	14	15	16	17
18	19	20	21	22	23	24
25	26	27	28	29	30	

22-24 Khuddam Ijtimaa | **29 - 30 Lajna Ijtimaa**

July		Wafa		Shawwal - Dhul-Qa'dah		
Mon	Tue	Wed	Thu	Fri	Sat	Sun
30	31					1
2	3	4	5	6	7	8
9	10	11	12	13	14	15
16	17	18	19	20	21	22
23	24	25	26	27	28	29

1 - Lajna Ijtimaa

August		Zahoor		Dhul-Qa'dah - Dhul-Hijjah		
Mon	Tue	Wed	Thu	Fri	Sat	Sun
		1	**2**	**3**	**4**	**5**
6	**7**	**8**	**9**	**10**	**11**	**12**
13	**14**	**15**	**16**	**17**	**18**	**19**
20	**21**	**22**	**23**	**24**	**25**	**26**
27	**28**	**29**	**31**	**31**		

September		Ikha		Dhul-Hijjah - Muharram		
Mon	Tue	Wed	Thu	Fri	Sat	Sun
					1	2
3	4	5	6	7	8	9
10	11	12	13	14	15	16
17	18	19	20	21	22	23
24	25	26	27	28	29	30

28-30 Jalsa Salana Tanzania

October		Tabook		Muharram - Safar		
Mon	Tue	Wed	Thu	Fri	Sat	Sun
1	2	3	4	5	6	7
8	9	10	11	12	13	14
15	16	17	18	19	20	21
22	23	24	25	26	27	28
29	30	31				

November		Nubuwwat		Safar - Raby'al-awal		
Mon	Tue	Wed	Thu	Fri	Sat	Sun
			1	2	3	4
5	6	7	8	9	10	11
12	13	14	15	16	17	18
19	20	21	22	23	24	25
26	27	28	29	30		

December		Fatah		Raby'al-awal - Raby'al-Thaany		
Mon	Tue	Wed	Thu	Fri	Sat	Sun
31					1	2
3	4	5	6	7	8	9
10	11	12	13	14	15	16
17	18	19	20	21	22	23
24	25	26	27	28	29	30

15 - 16 Ansarullah Ijtimaa

UPENDO KWA WOTE CHUKI SI KWA YEYOTE

Bustani ya Washairi

CHE MOSSE KATANGULIA (1950 – 2017)

Na Mahmood Hamsin Mubiru (Wamamba)

Kutoka Toleo lililopita

187. Kasi haikuwa nzuri
Akapewa tahadhari
Kutoka kwake Amiri
Muongozaji dunia.

188. Itachukua miaka
Shughuli kukamilika
Na sisi tuna haraka
Chapa hiyo kuitoa.

189. Nasi hatutasubiri
Na kwa hiyo ni dhahiri
Tutaipata dosari
Kazi tulojipangia.

190. Upesi kaacha kazi
Ili kuifanya kazi
Ni mapenzi yalo wazi
Rabbi Alompatia.

191. Kazi kaweka pembeni
Afanye kazi ya Shani
Watu hawakuamini
Kwa ile yake hatua.

192. Labbeka aliitika
Labbeka thumma labbeka
Huzur ninaitika
Sauti nimesikia.

193. Kusikia na kutii
Huo ni wetu uhai
Kupanda kwenye samai
Hilo la kuzingatia.

194. Vyote alitelekeza
Ili lengo kutimiza
Na maneno ya Muweza
Yaweze kuwafikia.

195. Sijui nitakula nini
Hakuweka maanani
Yeye kazi ya Manani
Ndiyo alofikiria.

196. Hakujali asilani
Cha kukiweka tumboni
Kakabidhi Rahmani
Riziki kumpatia.

197. Pasi na kutetereka
Shughuli ilifanyika
Bi. Khadija kadhalika
Kawa Khadija sawia.

198. Shem kafanya jihadi
Penye joto na baridi
Na kujenga ikisadi
Penye tundu kufukia.

199. Lugha pia kachangia
Maoni aliyatoa
Hivyo akasaidia
Upungufu kuondoa.

200. Akina mama hodari
Na kwa lugha ni mahiri
Wanaijua vizuri
Na sisi kutupatia.

201. Waalimu wa awali
Kutupa mwanga kamili
Kwa lugha wao kandili
Nuru kutuangazia.

202. Alijitoa mhanga
Ili ndani pawe mwanga
Kweli Mola kamkinga
Na yote yenye udhia.

203. Mchangowakeadhimu
Kamuwezesha Karimu
Upole na kuheshimu
Ikawa yake tabia.

204. Jukumu katekeleza
Na watoto kahimiza
Baba aliyoagiza
Waweze kuzingatia.

205. Hata nao auladi
Hawakukaa baidi
Walishiriki jihadi
Hali kuivumilia.

206. Yote walivumilia
Na kushukuru Jalia
Huku wakiomba dua
Lengo aweze fikia.

207. Neno liitwalo deko
Kwao wakasema mwiko
Wakaridhi kilichoko
Roho zao kutulia.

208. Raha ya kweli kinaya
Ukaridhika na haya
Kwako ikawa hidaya
Mikono ukainua.

209. Kukinai zao hali
Walichopata akali
Wakashukuru Jalali
Hicho walichopokea.

210. Si kila mara fulusi
Huleta raha halisi
Pengine ina mikosi
Chimbuko la mabalaa.

211. Hayo waliyamaizi
Wakaishika mizizi
Ni mizizi ya minazi
Ilo imara samaa.

212. Huo mfano mzuri
Wote wakawa tayari
Kuyatenda kwa hiyari
Bila yanguvu kutia.

213. Nyingi zikawa baraka
Kwao zikamiminika
Nyumba ikaneemeka
Kwa elimu na afua.

214. Baraka ziso idadi
Akazileta Wadudi
Kila namna zawadi
Nyumbani ikaingia.

215. Na kazi ikafanyika
Miaka mitano kufika
Ndipo ilikamilika
Kwa furaha na kwa dua.

216. Alikuwa habanduki
Alipokuwa hatoki
Na hata hiyo riziki
Mezani kumletea.

217. Ishirini kumi na tatu
Chapa ikafika kwetu
Furaha kwa kila mtu
Mwaka huo nakwambia.

218. Hakuna ya kuizidi
Kazi hino maujudi
Ina daraja kuzidi
Hino imetangulia.

219. Kaweka historia
Mtu wa pili tambua
Tafsiri kuitoa
Hapa kwetu Tanzania.

220. WakwanzaniMubaraka
Kwa Kiswahili kaweka
Maneno yake Rabuka
Nasi tukajipatia.

221. Ali Mosse ni wapili
Katuletea johali
Kitabu chake Jalali
Tukisome kwa wasaa.

222. Ni kwa lugha ya Kiyao
Tukalipata toleo
Zuri na lenye mng'ao
Roho zikafurahia.

223. Msamehe ya Khahari
Apate sehemu nzuri
Inukiayo uturi
Marashi ya kunukia.

224. Katu asiwe baidi
Na Mtume Muhammadi
Kamwe na wake Mahadi
Rabbi Alomteua.

225. Mpatie bustani
Ya majani ya kijani
Wapewayo Waumini
Maovu walokataa.

226. Kazi zilo maarufu
Nazo zenye utukufu
Qur'an ni Tukufu
Kwa cheo imezidia.

227. Daima tutakumbuka
Kazi hino ya baraka
Mikono itainuka
Kumkumbuka kwa dua.

228. Mpokelee Wadudi
Huyo mwana wa Saidi
Kwa hiyo yake juhudi
Tafsiri kuitoa.

229. Pepo ya Firdausi
Iliyojaa nemsi
Nayo apate nafasi
Thamarati kujilia.

230. Neema ilofuata
Ya kumsinga mafuta
Uamiri akapata
Khalifa kamteua.

231. Simu toka kwa Khalifa
Ikatupa taarifa
Mosse kapewa wadhifa
Ni Amiri Tanzania.

232. Katu sifanye ajizi
Huyo kwenu ni balozi
Msadi kwa kilia kazi
Mpate kuendelea.

233. Umma ukaitikia
Rabbeka tumesikia
Kushoto hata kulia
Msaada tutatoa.

234. Kuanza bismillahi
Dua hiyo akawahi
Yanapata usahihi
Unayoyakusudia.

235. Dua inaweka wazi
Ya kwamba wewe huwezi
Bila ya Mola azizi
Uwezo kukupatia.

236. Kiongozi mtumishi
Katu halina ubishi
Hakupata tashwishi
Yeye kujitutumua.

237. Alishika usukani
Na kuwa wetu rubani
Msaada kwa yakini
Yabidi kumpatia.

238. Utii unatakiwa
Ili lengo kufikiwa
Milango kufunguliwa
Wale wanonyenyekea.

239. Kazi kaanza kwa dua
Kumshukuru Jalia
Ili lengo kufikia
Na watu kutumikia.

240. Yanaipata baraka
Ya Mola wetu Rabuka
Kila kitu hunyooka
Kwani Mola karidhia.

241. Unakiri udhaifu
Pamoja na upungufu
Hivyo waomba Raufu
Aweze kusaidia.

242. Na katu hakuzuzuka
Wala kuzidi mipaka
Na hivyo hakuumbuka
Wadhifa kushikilia.

243. Mawazo alithamini
Walotoa waumini
Ofisi mkutanoni
Yote aliyapokea.

244. Sikio la kusikia
Rabbi Alimjalia
Makini alitulia
Na mwisho kuyapokea.

245. Watu wa zote tabaka
Wote waliheshimika
Maoni yao kashika
Na kazi kuyafanyia.

246. Mimi hapa mtumishi
Lingine kwenu sizushi
Ninaloomba tuishi
Jamaat kutumikia.

247. Kweli alitekeleza
Na mengi kuyatimiza
Kayaweka kwenye meza
Maoni kuyatolea.

248. Mushawarakwakedira
Hakufanya masikhara
Na wazo lililo bora
Hilo alilichukua.

249. Madaraka ni kileo
Huleta kubwa pumbao
Na kwa sababu ya cheo
Wengi ukawabeua.

250. Watu husahau kwao
Wakajiona ni mwao
Wakaweza na makwao
Mizizi kuipurua.

251. Kutembeakwamaringo
Kuweka hata kibyongo
Basi tena kwa uongo
Ni sasna wamezidia.

252. Cheo kikawa amana
Kaitunza na kufana
Mipaka kachunga sana
Kosa lisije tokea.

253. Aliweza changanyika
Watu wa kila tabaka
Kwani waliheshimika
Bila ya kuwabagua.

254. Kwelimapenzikwawote
Bila chuki kwa yeyote
Hilo ilikuwa pete
Sana aliitumia.

255. Kwa wote kuwa mlezi
Na akawa mtetezi
Ofisi ikawa wazi
Mwenye shida kuingia.

256. Kwenye Majisi Amila
Wajumbe hawakulala
Wakatekeleza mila
Taarifa kuzitoa.

257. Taarifa zilitoka
Mambo yalivyotendeka
Mijadala iliwaka
Maoni yao kutoa.

258. Makatibu wa idara
Kazi walitia fora
Wakafanya kwa ubora
Miiko kuzingatia.

259. Idara zikaamka
Wote wakachangamka
Na karatasi washika
Majibu wakiyatoa.

260. Majibu wakaelewa
Nini kilichotakiwa
Kweli walifanikiwa
Matunda kuning'inia.

261. Kila penye tofauti
Hakuweka tashtiti
Hiyo rehema ya dhati
Tofauti kutokea.

262. Ilikuwa changamoto
Ili kuongeza joto
Nao wingi wa fukuto
Ufanisi kuchochea.

263. Tofauti ni rehema
Kauli yake Hashima
Ina wingi wa neema
Kosa kuipuuzia.

264. Jambo zito la nidhamu
Kalifanya maalumu
Kwake ikawa muhimu
Na hatua kuchukua.

265. Kalipa kipaumbele
Ili kuondoa ndwele
Zilizoshamiri kule
Hata hapa biladia.

266. Nikaha nje Jamaati
Ikawa ni haihati
La kwanza upate hati
Ndipo itafungwa ndoa.

267. Tumeipata hasara
Kwa zile zetu harara
Ndoa pasipo tijara
Nje ya kundi sikia.

268. Watoto wamepotea
Kwa kuzifata tabia
Za watu walopotea
Jamaati kupuuzia.

269. Nanyumbanyingishabuka
Zimepata kuanguka
Jamaati imetoweka
Harufu hutosikia.

270. Hasarathammahasara
Tutaweka wapi sura
Bila ya kuwa imara
Wanajamati kulea.

271. Wengi tumewapoteza
Ni jambo linaumiza
Yabidi kutengeneza
Tusije kutumbukia.

272. Muumini wa kweli
Shimo moja mara mbili
Kudumbukia muhali
Mara ya pili tambua.

273. Elimu ilitolewa
Ya michango kuinua
Vipi inavyotakiwa
Si holela kuitoa.

274. Kutoa siyo khiyari
Kutoa hiyo amuri
Rabbi Ameikariri
Wamimma razaqnaa

275. Toa katika riziki
Alizokupa Maliki
Njia ya kutoa dhiki
Ambazo zakusumbua.

276. Tena kila ukitoa
Toa kilicho sawia
Kizuri cha kusifia
Sicho kilichosalia.

277. Sio kutoa makombo
Hapo utazua mambo
Toa kizuri cha umbo
Kizuri cha kusifia.

278. Utoaji ni wa siri
Utoaji ni dhahiri
Na njia hizi ni nzuri
Ni sawa yako nia.

279. Kutoa sawa na pato
Kama shamba au vito
Kinyume hiyo kushoto
Dhambi unajichumia.

280. Fedha bila ya risiti
Inatia wasiwasi
Kukuponya kwa upesi
Ni kanuni na sheria.

281. Somo likaeleweka
Michango kuongezeka
Na ile kubwa baraka
Ya kutoa wakajua.

282. Kutoa kuna baraka
Jambo limethibitika
Pato linaongezeka
Michango ukiitoa.

283. Matawi yakainuka
Hilo hasa ndilo shina
Likisimama mwanana
Matunda tutajilia.

284. Kweli yaliwezekana
Tukapanda na kuvuna
Tawi jambo la maana
Daraja la kuvukia.

285. Bila daraja huvuki
Na wala ng'ambo hufiki
Ulipokaa hutoki
Hujui kuogelea.

286. Yakapata uimara
Matawi yakawa bora
Nao wingi wa tijara
Faida ikatokea.

287. Tawi likawa mlinzi
Furaha hata simanzi
Ikawa ndiyo kurunzi
Giza lote kuondoa.

288. Tawi likakamilika
Habari likiandika
Habari ziso na shaka
Kamati zimepitia.

289. Matawi yakainuka
Shughuli kuchangamka
Na wafu wakafufuka
Uzima kujipatia.

290. Maraisi wa Mikoa
Nao hawakubakia
Hamasa na ushujaa
Sifa wakajichumia.

291. Kote wakahamasisha
Imani kuwazidisha
Yakajengeka maisha
Ya dini kuzingatia.

292. Wakawa wawajibika
Kwa yote yalofanyika
Katika yao mipaka
Kidini na kidunia.

293. Kweli hao maraisi
Wakawa wao ni rasi
Kuongoza kasikasi
Jamaati ikaenea.

294. Ikajitokeza nguvu
Ukaondoka uvivu
Pakatanda utulivu
Roho zilizotulia.

295. Umoja kweli ni nguvu
Yakatoka maumivu
Wakashikamana tuvu
Mema kuyatarajia.

296. Maraisi walivuma
Kwa matunda yalo mema
Yaliyotupa heshima
Kwa wale wasotujua.

297. Jamati hasa ni wewe
Ni mali yako mwenyewe
Na katu usiwe mwewe
Uchafu kujizolea.

298. Uliza kafanya nini
Jamati iwe mbioni
Kupambana na shetani
Maasi kuyaachia.

Endelea uk. 7

Kutoka uk. 6

CHE MOSSE KATANGULIA (1950 – 2017)

299. Hiyo yake falsafa
Wakaifanya ni dhifa
Wakataka hii sifa
Jamati kuitumia.

300. Semina kwa viongozi
Ili wapate ujuzi
Waepuke utelezi
Hata kazi kukosea.

301. Ilikuwa na faida
Kubwa kuliko ya rada
Matatizo hata shida
Yakawa yamepungua.

302. Watu mnapokutana
Mlifanyalo hufana
Na mawazo kupeana
Changamoto kutatua.

303. Na makala zikatoka
Ni nzuri za kusifika
Elimu kuongezeka
Watu wakajisomea.

304. Na silaha madhubuti
Inayong'ara katiti
Elimu ni hasanati
Thamarati kujilia.

305. Kutafuta ni lazima
Tena ufanye mapema
Si dhani imesimama
Dunia inakimbia.

306. Wajibu kuikimbiza
Usifanye kukawiza
Dunia huwaumiza
Nyuma wanaobakia.

307. Kuyamudu mazingira
Ukayajua saira
Cha kukupa uimara
Elimu kuzingatia.

308. Wajuzi na waso juwa
Ni katu hawawi sawa
Wenye elimu uluwa
Wasemalo huzamia.

309. Mosse alituhimiza
Lengo lino kutimiza
Elimu ina karaza
Kuna faida kujua.

310. Wanafunzi wa vyuoni
Walipata afuweni
Kwa kuipata auni
Ombi lao kupokea.

311. Shida walifafanua
Kwa amiri Tanzania
Mikopo inakawia.
Shida zinatuzidia.

312. Amiri akaandika
Barua akapeleka
Shida zinazowafika
Vijana wa Jumuia.

313. Khalifa kaidhinisha
Vijana wapewe falasha
Waweze kukamilisha
Kozi wanazochukua.

314. Hata hivyo hakupenda
Sehemu moja kupinda
Kitu alichokipenda
Matawi kutembelea.

315. Ukaaji Ofisini
Bila ya kutoka ndani
Hilo hakuliamini
Hupati uhalisia.

316. Alipenda kuondoka
Sehemu nyingi kufika
Ili aone hakika
Nini kinaendelea.

317. Hiyo elimu yakini
Unaelewa kiini
Toka juu hadi chini
Wajua pa kuanzia.

318. Ofisi wabahatisha
Kutoa wajumlisha
Huo mwendo unatisha
Ni rahisi kupotea.

319. Sehemu nyingi kufika
Kuwaona wahusika
Ni kweli kabahatika
Majuto yao kujua.

320. Kuambiwa na kuona
Tofauti kubwa sana
Usambe vinalingana
Kumi si sawa na mia.

321. Na kula wanachokula
Kalala wanapolala
Hakuchagua mahala
Kwa yeye kujibagua.

322. Kawa karibu na watu
Kweli akawa wa wote
Hakuwa baidi katu
Tufanyayo akijua.

323. Hizi zote harakati
Tukapata thamarati
Nidhamu kuidhatiti
Kwenye yetu Jumuia.

324. Barua za kukumbusha
Kwamba basi inatosha
Nao pasi ya kubisha
Hawakuweza rejea.

325. Wakaitoa ahadi
Kutofanya ukaidi
Kuyafanya yaso sudi
Bayati kuzingatia.

326. Kuzawa mara ya pili
Kwa ahadi ya Jalali
Hawatarudi mahali
Ni hapo walikokua.

327. Kondoo walopotea
Zizini wakarejea
Mchunga kawapokea
Ja mwana alopotea.

328. Hotuba misikitini
Nidhamu ni namba wani
Kukumbusha waumini
Kamba kuishikilia.

329. Kwenye jalisa salana
Kwa marefu na mapana
Mada zikafuatana
Nidhamu kuelezea.

330. Hata wakati wa shura
Ikasemwa ni kafara
Nidhamu iwe shakira
Tupate kuendelea.

331. Ulimwenguni hivi leo
Unahitaji video
Navyo vyombo vingineo
Habari kuturushia.

332. Dunia hii ya leo
Unahitaji redio
Navyo vyombo vingineo
Ujumbe wenu kujua.

333. Hivyo alivitumia
Vyombo hivyo kwa wasaa
Sauti ikaenea
Kotekote Tanzania.

334. Redio za mikoani
Kazitumia kwa shani
Ukatokea hewani
Ujumbe wa Ahmadia

335. Nazo za Daresalama
Akatumia hekima
"Jungu kuu" alisema
Watu wakatusikia.

336. Nahatakwenyeruninga
Amiri hakujivunga
Alikwenda toa mwanga
Giza lilipoenea.

337. Vyombohabarimuhimu
Vina nafasi adhimu
Kuelimisha kaumu
Tongotongo kuwatoa.

338. Hivyo akapata wazo
Kuanza mazungumzo
Tulipate nasi tuzo
Kituo kukifungua.

339. Zikaanza harakati
Kwenda kwenye daurati
Kusajili hadi cheti
Kituo kujipatia.

340. Tunatoa shukurani
Cheti tunacho kwapani
Twamshukuru Manani
Maombi kuyapokea.

341. Tayari tuna kituo
Ni karibu na gulio
Mtwara kuna upeo
Kusini kuendelea.

342. Katika huno mradi
Ali Mwana wa Saidi
Mchango wake zaidi
Na mawazo kuchangia.

343. Mchango wake kabili
Aupokee Kahali
Malipo yake mazuli
Viumbe twamuombea.

344. Msingi ameuweka
Mola twaomba baraka
Malipo yalotukuka
Yaweze kumshukia.

345. Tunakuomba Karimu
Sauti ya Islamu
Redio yetu adhimu
Mafundisho kuyatoa.

346. Islamu hasa nini
Tueleze kwa makini
Islamu ni amani
Daima kunyenyekea.

347. Kuishi na majirani
Kwa mapenzi na hisani
Bila shari asilani
Mmoja kumchukia.

348. Mapenzihasakwawote
Bila chuki kwa yeyote
Hiyo kwetu iwe pete
Kuvaa bila kuvua.

349. Kwamba jihadi upanga
Ni funzo wamebananga
Tuwape waone mwanga
Gizani kuto bobea.

350. Utume waendelea
Na ushahidi kutoa
Ili waweze tambua
Utume ndio shufaa.

351. Nabii Isa afile
Acheni visa vya kale
Anayeishi milele
Si mwingine ni Jalia.

352. Italeta mapinduzi
Akishapenda azizi
Italeta mageuzi
Kwa hamu twasubiria.

353. Kazi nyingine adhimu
Ujengaji maalumu
Ukumbi wenye nudumu
Ukhalifa kumbukia.

354. Juhudi zilifanyika
Za ukumbi kujengeka
Kuikumbuka baraka
Mola Alotupatia

355. Hiyo alama tukufu
Kwa wa leo na halafu
Watasimama kwa safu
Shukurani kuzitoa.

356. Ali Mwana wa Saidi
Alikuwa na juhudi
Kuanzisha makusudi
Taasisi za jamia.

357. Zisizo za serikali
Zao wajasiriamali
Alianzisha kwa hali
Umasikini kutoa.

358. Pia akawashauri
Ufugaji kwa hadhari
Kuku wapate wazuri
Faida kujipatia.

359. Elimu kaitumia
Kwa ajili ya jamia
Wengi walifurahia
Elimu aliyotoa.

360. Vitabu aliandika
Viwili navikumbuka
Kuhusu fedha hakika
Na cha miradi kujua.

361. Kilele cha mafanikio
Hayo tuonayo leo
Kitonga ndio upeo
Hapo tulipofikia.

362. Uamuzi wa busara
Uamuzi ulo bora
Uamuzi wa tijara
Wa sisi kujikomboa.

363. Uamuzi namba wani
Umetupayo auni
Shukurani kwa Manani
Wazo Alotupatia.

364. Ni uamuzi wa m waka
Sote tumeneemeka
Ni uamuzi wa baraka
Sasa tunajitambua.

365. Kitonga yetu kitonga
Tunafurahi wahenga
Na vijana wametinga
Wote tukifurahia.

366. Kitonga ni bustani
Panapendeza machoni
Upepo wake jamani
Kwa madaha wapepea.

367. Kitonga ina wasaa
Huwezi kufa na njaa
Pana rutuba ajaa
Kilimo kujilimia.

368. Pana nafasi yatosha
Majengo kusimamisha
Kitonga kweli yatisha
Twamshukuru Jalia.

369. Msingi aliyeweka
Ya Kitonga ya baraka
Wajibu kumkumbuka
Na dua kumuombea.

370. Kumsahau vigumu
Kwa kazi ile adhimu
Kutupatia makamu
Kitonga tumetulia.

371. Kuku aliye mgeni
Ana kamba mguuni
Kwa sasa aliwatani
Kamba tumeshaitoa.

372. Tumekuwa ni wenyeji
Tena tunatoa mtaji
Na mengi tunataraji
Lengo letu kufikia.

373. Kutuletea heshima
Na uwingi wa adhima
Leo tunayo salama
Chako ni chako sikia.

374. Leo tunatabasamu
Hapa tumestakimu
Twamshukuru Karimu
Neema kutupatia.

375. Kwako ni kwako jamani
Hata kama ni pangoni
Kitonga kwetu nyumbani
Nani wa kutusumbua?

376. Zamani tulisumbuka
Tusipate pa kushika
Ilikuwa patashika
Shida ya kuendelea.

377. Kila ukifika mwaka
Barua tunaandika
Zayo nafasi kuweka
Tuwezapo kutumia.

378. Tulipigwa danadana
Na la kufanya hatuna
Kama huna yako zana
Lazima utaumia.

379. Mtu chake walisema
Maneno yenye hekima
Na kile cha kuazima
Watakuja kichukua.

380. Na kweli tuliumia
Kutangatanga na njia
Heshima ikapotea
Dharau kukithiria.

381. Kujua tulikotoka
Ni jambo lilotukuka
Uendako hutofika
Pasi nyuma kupajua.

382. Kujua unakotoka
Ni jambo limenyooka
Mabaya utaepuka
Muhali kuyarudia.

383. Kidogo turudi nyuma
Tuyafahamu ya zama
Sababu sisi kuhama
Na Kitonga kuingia.

384. Zilikuwepo sababu
Sasa ninao wajibu
Wa mimi kuzikutubu
Wajao kukumbukia.

385.Miakatwendemiakarudi
Tena hata na zaidi
Kilio tulikinadi
Sisi shule kufungua.

386. Agenda zote za shura
Tena bila masikhara
Na kwa sauti imara
Shule tunatarajia.

387. Hata na sisi kwa sisi
Kwa uwazi si tetesi
Tulisema pasi wasi
Shule tunaiwazia.

388. Bila shule ni maafa
Tutakosa maarifa
Katika hili taifa
Tutaushika mkia.

389. Hapa chini ya samau
Wengi watatudharau
Na hata kutusahau
Kama sisi ni raia.

390. Akiwa madarakani
Mosse alilibaini
Hili jambo la thamani
Haraka kulitatua

391. Linataka ufumbuzi
Bila kufanya ajizi
Lolote hatuliwezi
Pasi shule kuzindua.

392. Kwa ruhusa ya Amiri
Tulifanya tabasuri
Tukakutana tayari
Mipango kujipangia.

393. Kujenga shule ni vita
Sio jambo la kuota
Ni harambe na kuvuta
Shabaha kuifikia.

394. Barua tulisambaza
Za wajumbe wa baraza
Madhumuni kueleza
Kilo tulokusudia.

395. Wajumbe wakaitika
Sote tukakusanyika
Msikiti wa baraka
Wajumbe kuhudhuria.

396. Ni Masjid Salaam
Tukiwa na tabasam
Tukazitoa salam
Bila hata kukawia.

397. Saba ni mwezi wa tano
2006 ndio mwaka wa mavuno
Vikatarishwa vinono
Na mengi yakatokea.

398. Amiri kahutubia
Machache kutuambia
Mikakati kuibua
Na shule kujijengea.

399 Kutumia nguvu zetu
Pamoja na watu wetu
Chochote kilicho chetu
Twaweza jitegemea.

400. Bila kujitegemea
Hupati kuendelea
Na hiyo ndio sheria
Rabbi alotuumbia.

401. Alobaki ni Katibu
Kikao kukiratibu
Mambo yakawa twaibu
Wajumbe wakatongoa.

402. Ni katibu wa elimu
Aliyopewa jukumu
Ili kuchunga nidhamu
Madhumuni kufikia.

403. Akawaambiawajumbe
Maneno mengi ukembe
Ahadi hasa ulumbe
Ni kipi utakitoa.

404. Hatuhitaji maneno
Maneno sio msuwano
Matendo yawe kivuno
Haya tunatarajia.

405. Kasimama Sultani
Kasema twende shambani
Nalitoa kwa Manani
Shule tupate inua.

406. Njoni kulitazama
Kama tafaa azama
Na tuone hima hima
Vifaa kuvinunua.

407. Ungandokawashamoto
Kawaamsha watoto
Nao wakapata joto
Ahadi kututajia.

408. Kasimama na Malinda
Neno moja hakupinda
Ahadi iliyowanda
Saruji katupatia.

409. Tani moja ya saruji
Na mengine mahitaji
Inshallah anataraji
Kamati kuipatia.

410. Kaja Yunus wa Haji
Kaamba ana mtaji
Anajua ujengaji
Shule atatujengea.

411. Ahadi ya madawati
Kazema kajizatiti
Ayatoe kwa wakati
Wakati ukiwadia.

412. Wote walohudhuria
Na ahadi walitoa
Ili iweze timia
Dhamira yetu na nia.

413. Kuisha hicho kikao
Tukaenda mbio mbio
Taarifa za kilio
Na sababu za kulia.

414. Yote tukamueleza
Bila moja kubakiza
Na yeye kasikiliza
Na shukrani kutoa.

415. Amiri akatutuma
Kitonga twende kwa hima
Tutizame na kupima
Iwapo panafalia.

416. Labeika tukaitika
Tukaenda kwa haraka
Amiri akitamka
Yabidi kuitikia.

417. Utii kwake Amiri
Ni lazima na amuri
Ni agizo la Bashiri
Usia katuachia.

418. Safari yetu watatu
Kwenda kuona msitu
Sheikh Ame ni mwenzetu
Kiongozi alikuwa

Itaendelea toleo Lijalo

Mapinduzi ya Kujitolea Mali katika njia ya Allah yaliyoletwa na Masihi Aliyeahidiwa a.s.

Kutoka Toleo lililopita

Mada iliyotolewa kwenye Jalsa Salana 2017 na:

Abdulrahman M. Ame sahib

Kwanza ninukuu mifano michache ambayo Masihi Aliyeahidiwa a.s. yeye mwenyewe aliwahi kuitaja.

Katika kitabu chake cha *'Ushindi wa Islam'*, Masihi Aliyeahidiwa a.s. akitaja kiwango cha kujitolea cha masahaba zake anaandika:

Kwanza kabisa ninacho kiherehere moyoni mwangu cha kumtaja ndugu yangu mmoja wa kiroho, anayeitwa jina Nurdin (sawa na nuru ya ikhlasi yake). Mimi daima namtazama kwa macho ya kumwonea wivu kutokana na baadhi ya huduma zake za kidini anazofanya kwa kutumia mali yake ya halali, kwa ajili ya kushindisha neno la Islam, kwamba laiti huduma hizo ningeweza kuzifanya nami pia.

Akizidi kuandika anasema:

Naandika hapa mistari michache ya baadhi ya barua zake kama mfano ili wasomaji wafahamu kwamba ndugu yangu mpendwa Maulawii Hakim Nuruddin wa Bhera, tabibu wa serikali ya Jammu, ameendeleaje mbele sana katika madaraja ya upendo na ikhlasi. Na mistari yenyewe ndiyo hii:-

Maulana, Mwongozi wetu, Imam wetu, Assalamu alaikum wa rahmatullahi wa barakatuhu. Mheshimiwa, naomba dua kwamba saa zote niwe pamoja nawe, nikapate kutoka kwa Imamu wa zama matilaba ambayo kwayo amefanywa kuwa Mujaddidi. Kama ningeruhusiwa, ningejiuzulu kazi na ningeshinda kwako usiku na mchana. Au kama nikiamriwa niondoke na kuzunguka duniani kote na kuwaita watu kwenye dini ya haki na kufia katika njia hii. Nimejitolea kwako. Chochote nilicho nacho si changu, ni chako. Mheshimiwa Mwongozi wangu, nasema kwa kweli kabisa kuwa ikiwa mali yangu yote itumike katika kueneza dini, nitapata shabaha yangu. Kama wale waliotoa mapema bei ya kukinunua Barahin wana wasiwasi kwa kuchelewa kwa uchapishaji wa kitabu, basi niruhusu mimi nitoe huduma hii ndogo ya kuwarudishia bei yao yote waliyokwisha toa. Mheshimiwa mwongozi wangu! Mimi niliye mzembe na mnyenyekevu nasema, ukikubali nitakuwa na bahati njema, kwamba ningependa gharama zote za uchapishaji wa Barahin ziwe juu yangu, na kiasi chochote kitakachopatikana kwa mauzo yake, fedha hizo zitumike kwa mahitaji yako. Nina uhusiano na wewe Kifaruki, (kama Seyyidna Umar Faruk alivyohusiana na Mtume s.a.w) niko tayari kutoa kila kitu katika njia hii, niombee mauti yangu yawe mauti ya Masiddiki.

Katika kitabu hicho hicho Masihi Aliyeahidiwa a.s. anaendelea kuandika:

Rafiki mwingine ni ndugu Hakim Fadhl Din wa Bhera. Bwana Hakim msifiwa, kiasi alicho nacho kwangu cha upendo, ikhlasi, itikadi njema na uhusiano wa ndani, nashindwa kueleza. Yu mtu mwenye kunitakia mema kikweli, kunihurumia kwa moyo na mwenye kutambua ukweli wa mambo. Baada ya Mwenyezi Mungu kunielekeza kuandika kijitabu hiki na kunipa matumaini kwa funuo zake makhsus, niliwaeleza watu kadhaa kugharamia uchapaji wa kijitabu hiki, lakini hakuna yeyote aliyeafikiana nami. Lakini ndugu yangu mpenzi, pasipo mimi kumwambia, akanihamasisha mwenyewe kuandika kitabu hiki na akatoa rupia mia moja kwa ajili ya kukigharamia. Nastaajabia busara yake ya kiimani kwamba dhamira yake imeenda sambamba na dhamira ya Mwenyezi Mungu. Daima hutoa huduma kwa siri, na amekwisha toa rupia mia kadhaa kwa siri katika njia hii, kwa ajili tu ya kutafuta radhi ya Mwenyezi Mungu. Mwenyezi Mungu na Ampatie malipo mema.

Hadrat Khalifatul Masih II (ra) anasimulia tukio lifuatalo kumhusu Hadhrat Munshi Arora Sahib (ra):

Miezi michache baada ya kifo cha Masihi Aliyeahidiwa a.s., Munshi Sahib alifika nyumbani kwangu. Mtu mmoja alikuja kuniambia kwamba kuna mtu mlangoni ananisubiri. Nilipotoka nje nikamuona Munshi Arora Sahib ndiye anayenisubiri. Baada ya kupeana mikono ya kusalimiana kwa bashasha akatoa paundi chache kutoka mfukoni mwake na akaniomba nimpatie Hadrat Ammān Jan [mke wa Masihi Aliyeahidiwa a.s.]. Mara tu alipomaliza maneno hayo, akaanza kulia sana tena kwa sauti. Baada ya muda kidogo alipotulia nilimuuliza ni nini kimlizacho? Akasema wakati nilipokuwa maskini nilikuwa naweza kusafiri kuja Qadian muda wowote nilipopata likizo.

Nilikuwa naanza kutembea kwa miguu hadi Qadian ili niweze kuokoa baadhi ya fedha na nimpatie Masihi Aliyeahidiwa a.s.. Nilipofika hapa nikawaona matajiri wakichangia kiasi kikubwa kwa ajili ya imani, nami nikapenda kutoka moyoni mwangu, kwamba kama ningekuwa na fedha za kutosha, ningechangia vipande vya dhahabu badala ya fedha kwa Masihi Aliyeahidiwa a.s.. Hatua kwa hatua, mshahara wangu uliongezeka (wakati huo mapato yake yalikuwa kiasi cha rupia 20-25) na nilianza kuhifadhi pesa kila mwezi kwa lengo kwamba kama nikifikia lengo langu basi nizibadilishe kuwa paundi na hatimae niweze kumpatia Masihi Aliyeahidiwa (as).

"Kama kiwango kilifikia kiasi cha kubadilisha kuwa pauni



Abdulrahman M. Ame sahib

moja, nilikuwa nikizibadilisha na kupata Paundi, kisha nilianza kukusanya tena. Niliendelea kurudia hivi mpaka nikaridhika kwamba kiasi cha Paundi nilichopata kinatosha sawa na nia yangu. Baada ya kusema hayo hakuweza kujizuia na akaanza kulia tena. Baada ya muda, hatimaye alipokusanya nguvu za kutosha, alisimama kulia na kusema kuwa sasa ninazo fedha za kutosha lakini Masihi Aliyeahidiwa a.s. (as) ameshafariki. Mtu anaweza kusoma katikati ya mistari hii, ni kubwa kiasi gani ilikuwa jazba ya kujitolea ya sahaba huyu maskini wa Masihi Aliyeahidiiwa a.s.

Pia Hadhrat Khalifatul Masih II (ra) ameandika:

Katika zama za Masihi Aliyeahidiwa a.s. ambapo kulikuwa na mashtaka mengi yaliyokuwa yakiendelea huko Gurdaspur, kuliibuka haja ya ziada ya fedha. Masihi Aliyeahidiwa a.s. aliweka ombi hili mbele ya rafiki zake na masahaba zake kwamba kwa vile Langar Khana ilikuwa imefunguliwa sehemu mbili yaani (Qadian and Gurdaspur), na ukiongeza kwamba fedha zilikuwa zinatumika kwa ajili ya kesi, hivyo kuna haja kubwa ya marafiki kuweka fikra zao zaidi juu ya kujitolea mali.

Kwa bahati tu ikatokea, Dr. Khalifa Rasheed ud Din Sahib akapata kujua juu ya ushauri huo wa Masihi Aliyeahidiwa a.s. katika siku ambayo alikuwa amepokea mshahara wake wa Rupia 450. Hapo hapo akautuma mshahara wake huo wote kwa Masihi Aliyeahidiwa a.s. Wakati rafiki yake mmoja alipomwambia ingekuwa vizuri kama ungebakisha kidogo kwa ajili ya matumizi yako ya nyumbani, Dr. Sahib akajibu, "Inawezekanaje mimi nibakishe chochote kwa ajili ya matumizi yangu wakati Khalifa wa Mwenyezi Mungu ananiambia ana mahitaji kwa ajili ya Dini Yake Allah? Angalia ni nini hiki kama sio mapinduzi yale yale waliyoyapata akina Abubakar r.a!

Hii ni mifano michache tu lakini kwa hakika maswahaba wa Masihi Aliyeahidiwa a.s. na wafuasi wake wa baadae wamepata mapinduzi makubwa ya uelewa kwamba kujitolea huku hakukutakiwa kukatike kwani wao walikuwa wamekabidhiwa kazi ya kuusambaza Uislamu duniani kote.

Hivyo hata baada ya kufariki kwa Masihi Aliyeahidiwa a.s., kupitia Makhalifa wake sifa hii ya kujitolea imeendelea kukua kwa hali ya ajabu na kushangaza. Sote tunakumbuka kwamba baada ya tukio la wale waliokataa kuchukua baiat ya Hadhrat Musleh Mauud kuwa Khalifa wa pili, waliondoka na kila kitu na kuacha senti chache tu kwenye mtoto wa meza, lakini Allah Aliibariki Jamaat kwa watu wenye moyo wa kujitolea kaisi hiki kwamba haijawahipo kutokea katika Jumuiya hii haja ya kweli na ikashindikana kutekelezwa kwa sababu ya ukata au ufukara, na Inshallah haitotokea hivyo daima.

Mnamo mwaka 1934 wakati Hadhrat Khalifatul Masih II r.a. alipoanzisha mpango wa Tahrik Jadid, mifano ya ajabu ya kujitolea, iliyojaa hamasa na jazba za kiimani inayong'aa kama nyota za angani, inayomuwacha mtu akipigwa na butwaa juu ya mapinduzi makubwa ya kujitolea mali yaliyoletwa na Masihi Aliyeahidiwa a.s. ndani ya wafuasi wake hawa ambao wengi wao hawakuwepo wakati wa uhai wake.

Hadhrat Mirza Tahir Ahmad, Khalifatul Masih IV r.a. katika hotuba yake ya Ijumaa ya Nov. 5 1982 anaueleza mpango huu wa Tahrik Jadid ulivyoanza kwa maneno yafuatayo:

Kwa hiyo ni kwa misingi hii kwamba Hadhrat Musleh Ma'ud (ra) alitangaza kuundwa kwa mpango huu mwaka 1934. Kwa kuzingatia hali ya kiuchumi ya wakati huo na umaskini wa jamii, alifanya wito wa rupia 27,000 tu. Hata hivyo hisia zake ni kwamba hali ya kiuchumi ya Jumuiya isingeweza kudumisha mzigo huu kwa muda usiojulikana. Kwa maneno mengine, hali ya uchumi ilionekana kulazimisha kwamba mpango huu lazima usitekelezwe kwa kudumu na badala yake dhabihu hii iombwe kufanyika kwa miaka michache tu. Kwa hiyo, alitangaza kwamba mpango huu utakuwa ni wa miaka 3 ambayo kwa kupitia huo uenezi wa Uislamu ungetekelezwa katika dunia nzima. Wakati huo, watu hawakuelewa kikamilifu hatua hii. Kulikuwa na wengi ambao walidhani kwamba mpango huu ni kwa ajili ya mwaka mmoja tu. Kwa hiyo, wao wakaahidi michango yao ambayo ilikuwa nje ya uwezo wao. Baadhi ya makarani waliokuwa wakifanya kazi kwa ajili ya Jumuiya ambao walipata rupia 15 tu kwa mwezi waliahidi kiasi cha mchango sawa na mishahara yao ya miezi mitatu. Wengine waliahidi mishahara yao ya miezi 2 wakifikiri kwamba watakuwa wamelipa ahadi zao katika kipindi cha mwaka mmoja au miwili.

Baadhi ya wazee wa Jumuiya ambao walikuwa na mishahara bora kidogo,ingawaje bado mishahara yao ilikuwa ni midogo sana ikilinganishwa na viwango vyovyote vya kidunia. Kwa mfano, watu ambao walikuwa na kiwango cha wakurugenzi [Naziran], na wafanyakazi wa mwanzoni na masahaba wa Masihi Aliyeahidiwa a.s. ambao waliwahi kuitumikia Jumuiya kwa muda mrefu sana walikuwa na mishahara isiyozidi rupia sitini au sabiini kwa mwezi. Kwa mfano, Hadhrat Mufti Muhammad Sadiq Sahib (ra) aliahidi rupia mia mbili na hamsini. Vile vile, Sheikh Abul Atta Sahib (aliyekuwa mdogo sana wakati huo) na Hadhrat Sheikh Jalal Uddin Sahib Shams, wote waliahidi rupia 50-55 ambazo zilikuwa ni zaidi ya uwezo wao.

Wakati huo haikuwa wazi sana kwamba mpango huu ni wa kudumu kwa asili. Lakini, baadaye, kwa uwazi ilipotangazwa kuwa mpango huu ni kwa miaka mitatu na si kwa ajili ya mwaka mmoja, hakuna hata mtu mmoja aliyejitokeza na kuomba kwamba alikuwa ameahidi kiasi fulani kimakosa na kwamba ipunguzwe kwa sababu ilikuwa ni zaidi ya uwezo wake kutimiza. Kwa upande mwingine, Hadhrat Musleh Maud (ra) mwenyewe alitangaza kuwa kama mtu amefanya ahadi kwa sababu ya kutokuelewa basi anaruhusiwa kutathmini ahadi yake. Katika majibu ya tangazo hili, alipokea barua mbalimbali kutoka kwa wanajumuiya wakisema kuwa wanaomba waruhusiwe kuendelea na ahadi zao, nao walimuomba awaombee ili waweze kutimiza ahadi zao. Lakini hakuna hata ombi moja lilipokelewa la kuomba ahadi zao kupunguzwa. Baadaye, wakati ilipokuwa wazi zaidi kuwa mpango huu sio tu kwa miaka mitatu bali ni wa kudumu na mpango mkuu wa njia ambayo ujumbe wa Masihi Aliyeahidiwa a.s. utafikishwa pembe zote za dunia, hata baada ya tangazo hilo hakuna hata mtu mmoja aliyerudi nyuma badala yake waliendelea kusonga mbele kujitolea dhabihu. Hii ilikuwa ndio hali ya wazee; hii ilikuwa ndio hali ya matajiri; watu wa kundi la kati ambao walikuwa si watumishi wa Jamaat moja kwa moja nao pia walikuwa na hali hiyo hiyo, maskini nao walikuwa na hali hiyo hiyo. Kila sekta ya Jumuiya nzima wakajitokeza kwa pamoja ili kujitolea kafara. Na leo uchambuzi wa takwimu hauwezi tueleza hasa ni sehemu gani ya Jumuiya ilijitolea sadaka zaidi kuliko nyingine. Matajiri walichukua hatua kubwa kulingana na uwezo wao. Waliahidi kiasi kikubwa kwa moyo wote [si kwa maneno tu] na kisha walitimiza ahadi hizi kwa neema ya Mungu. Vile vile maskini walishiriki katika mpango h uu kulingana na uwezo wao, bali kwa hakika zaidi ya uwezo wao. "

Itaendelea toleo Lijalo, Inshallah.

Tunalo Somo katika Maisha ya Mzee Sultan Ungando

Kutoka uk. 4

FUNUNU YA JUMUIYYA

Mzee Sultani Mohammed Ungando alipokuwa hai, nilifanya naye mazungumzo nyumbani kwake kule Tandika. Ilikuwa mnamo tarehe 24/10/2007. Aliniambia kwamba mnamo mwaka 1953, alipokuwa kule Ifunda kwenye shule ya Ufundi, kulikuwa na mwanafunzi mwenzao mmoja akiitwa Masud Abdullah Msolomi. Huyu aliwaambia kuwa kuna watu wanaoitwa Makadiyani. Hao bwana wanaijua sana Qur'an Tukufu, kwa kuisoma, tafasiri na kuitolea maelezo. Wana hoja zisizojibika. Wana maelezo ya kueleweka. Hao wameweza kumchukua mdogo wake Jaafari Abdullah Msolomi. Makadiyani ni watu wa khatari, kama si makini watakuchukua mara moja maana ni mafaswaha wa maelezo. Baadaye Mzee Sultani Ungando aliniambia kwamba siku moja alisoma kwenye gazeti moja lililokuwa linatolewa kule Kenya kwa lugh aya Kimombo likiitwa "East African Standard" kwamba "Sasa Qur'an Tukufu yenye juzu 30, Sura 114 imetafsiriwa kwa lugha ya Kiswahili na Jumuiyya ya Ahmadiyya. Mzee Sultani Ungando aliniambia pia kuwa alipozisoma khabari hizo alifurahi sana. Aliendelea kunieleza kuwa alimshukuru mno Mwenyezi Mungu ijapokuwa alikuwa bado hajaisoma hiyo Tafsiri yenyewe wala kuiona. "Sikiliza bwana mdogo, Mzee Ungando aliniambia katikati ya mazungumzo yetu, "Nilimshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa sababu ya kukubali kilio chetu cha siku nyingi cha kupata Tafsiri ya Qur'an Tukufu kwa lugha ya Kiswahili iliyotafsiriwa na Waislam wenyewe"

Mzee Ungando ameipitia Tafsiri ya Qur'an Tukufu iliofanywa na Padre Dale. Aliniambia nilipoisoma niliudhika sana kwa ile kauli yake ya kulinganisha Qur'an Tukufu na Biblia. Padre Dale kwenye maandiko yake hayo ameandika kwamba; "Qur'an ni sawa na kibatali na Biblia ni ni karabai. Hata hivyo Mzee Ungando khabari alizozisoma kwenye 'East African Standard' zilimsisimua sana. Akapeleka taarifa hizo kwao Rufiji kwa hamu na shauku kubwa. Lakini jibu lilikuwa kinyume na mtazamo wake. Jibu lenyewe lilikuwa la kumuonya na kumtahadharisha kwamba asiwe nayo karibu, asiisome wala asiikumbatie Tafsiri hiyo kama ataiona. Ndugu zake walimwambia kwamba tafsiri hiyo imeleta mgogoro mkubwa sana baina ya Masheikh. Pamoja na hayo, mtu mmoja alimwandikia Mzee Sultani Ungando kwamba yeye amepata kuisoma Tafsiri hiyo. Alimtaarifu kuwa Tafsiri hiyo imetolewa na Jumuiyya ya Waislam wa Ahmadiyya. "Ukiacha ile Tafsiri ya Padre Dale, lakini hii pia ndani yake kimetumika Kiswahili fasaha ajabu. Maneno yaliyomo ndani yake si ya kawaida. Haikosi mtu aliyetafsiri kwa kweli huenda akawa walii wa Mungu". Hii ilikuwa sehemu ya barua aliyokuwa ameandikiwa Mzee Sultani Ungando kutoka kwa nduguye huyo. Ni maelezo mawili tofauti aliyopewa Mzee Ungando. Lakini mnamo mwaka 1954 akiwa kule Mkoani Lindi, Mzee Ungando ndiko alikopata khabari kamili za Ahmadiyya tena kwa makini kabisa. Kwa wakati ule Wanajumuiyya wa kule waliwahi kufanya majadiliano na Sheikh maarufu wa huko akiitwa Mohammed bin Yusuf. Kwenye majadiliano hayo, Sheikh Mohammed bin Yusuf alihemwa sana na alikuwa anashindwa kujibu maswali kadhaa aliyokuwa anaulizwa na Waahmadiyya.

Ilipofikia hapo, mwanafunzi mmoja wa Sheikh Mohammed bin Yusuf alichukuwa kitabu cha Safina ya Nuhu kilichoandikwa na Seyidna Ahmad (as) na kuwasomea watu. Aliwasomea ile sehemu inayosema kwamba watu watakapoanza kufanya makosa, Mwenyezi Mungu Atateremka Mwenyewe kuja kupambana na watu. Mwanafunzi yule akawauliza wasikilizaji wake, je hayo maneno mliyoyasikia si ya ukafiri? Kufikia hapo zogo likaanza na vurugu kubwa ikafanyika na polisi walifika kutuliza rabsha hiyo. Wakati huo wote Mzee Ungando alikuwa bado hajajiunga na Ahmadiyya. Mzee Ungando alipokuwa Lindi alikuwa anatembelewa na mtu mmoja mtanashati na nadhifu sana. Mtu huyo alipenda kuvaa vazi jeupe. Yaani, alikuwa anavaa sarawili nyeupe, shati jeupe, akivaa kanzu, basi inakuwa nyeupe na kofia alikuwa anavaa nyeupe. Mzee Ungando aliwauliza wenyeji wake pale alipokuwa anakaa, yule mwenye vazi la nyangenyange alikuwa nani? Anapenda mno kuzungumza mambo ya dini wakati wote. Wenyeji nao wakamuuliza mtu huyo yukoje? Mzee Ungando akawaelezea alivyo. Wenyeji wake wakamweleza kwamba huyo ni Sheikh Ahmad Mataka Busra, ndiye Kadiyani mkubwa na hii nyumba unayoishi wewe ni ya ami yake. Mtu mwingine alimwambia Mzee Ungando kwamba atanabahi sana na huyo mtu anayemuita mtanashati. Si mtu mwema ni kafiri ana mtume wake. Ukimzowea atakuingiza katika ukafiri wake na kuacha Uislamu wake. "Mimi ninamvizia siku moja nitamcharaza mikwaju". Lakini kabla ya kutekeleza nia hiyo, bwana huyo alipewa uhamisho wa kwenda Dar es salaam kufuatana na utaratibu wa kazi yake ulivyokuwa.



THE CMC Motors yesterday awarded a two band *Philips* radio cassette plus 100,000/- cash to Ndugu Sultani Mohamed Ungando who retired on November 1, this year after working for the company for 35 years.
The prizes which are besides Ndugu Ungando's retiring benefits were presented to the former Service Advisor with the company, Ndugu Ungando by the CMC Managing Director, Ndugu Abdul Haji during a brief ceremony held at the company workshop Chang'ombe area in Dar es Salaam yesterday.
Ndugu Ungando advised CMC workers to abide by the working discipline, commitment and avoid theft towards becoming good employees for the interest of the company.
Above, Ungando (left) receiving his prizes from Ndugu Haji while looking on are some CMC Motors senior officials.

Mzee Sultan M. Ungando akikabidhiwa zawadi ya raedio na Tsh. 100,000 wakati alipostaafu kazi kutoka kampuni ya magari ya Cooper motors mwaka 1991

Labda ni mpango wa Allah. Baada ya kuondoka Lindi bwana mkubwa huyo, Sheikh Ahmad Mataka akawa amepata wasaa mpana sana wa kumhubiri Mzee Ungando. Mzee Sultani Ungando akaondowa woga wa kuwaogopa Masheikh wake wa Kisuni akawa tayari sasa kusikiliza maelezo ya Ahmadiyya. Sheikh Sharma kutoka Dar es salaam alipofika Lindi, Sheikh Mataka alimuunganisha na Mzee Ungando kuzungumzia ujaji wa Seyidna Ahmad na uanzishwaji wa Jumuiyya ya Ahmadiyya. Kwa kimaandishi Mzee Ungando aliunganishwa na Maulana Muhammad Munawwar akiwa Nairobi Kenya. Miongoni mwa maandiko ya Sheikh Munawwar kwenda kwa Mzee Ungando alimwandikia akisema kuwa "Si sawasawa kumsifia baba yako yu shujaa anapopigana na simba mlangoni na wewe mtoto unafunga mlango wa chumba chako". Kwa maandiko ya kauli hiyo, mzee Ungando alielewa anatakiwa kufanya nini.

Basi mzee Sultani Ungando akaendelea kusikiliza mahubiri ya Ahmadiyya kwa makini zaidi. Kwa mara ya kwanza sasa akanunua tafsiri ya Kurani tukufu kwa Kiswahili toleo la kwanza kwa shilingi 30/= ambalo mpaka anafariki alikuwa analo.

Mzee Sultani Ungando aliondoka Lindi na kuja Dar es Salaam. Alipenda sana kujua khabari za yule nduguye aliyekuwa naye kule Lindi na kuhamishiwa Dar es Salaam kikazi. Akauliza uliza kisha akaambiwa bwana huyo amekwenda Rusende kule Rufiji. Kwa kuwa babu mdogo wa mzee Ungando alikuwa anaishi upande huo, mzee Sultani akapatwa hamu ya kufika huko kuwaona wote wawili.

Naam, mzee Sultani Ungando Mungu Bariki alijaaliwa kufika Rusende kule Rufiji kwa babu yake. Yule bwana aliyekuwa anamtafuta aliishi kijiji cha pili ambacho kilikuwa kinaitwa Nyipara, lakini aliposikia anatafutwa na mzee Sultani Ungando, naye akajitahidi wakutane. Basi Mwenyezi Mungu akawakutanisha. Ni mzee Sultani Ungando na mzee Mbwana Shamte Nyengo. Ahlan, wasahalan, khabari za siku nyingi. Waliulizana khabari za siku, tangu pale walipoachana kule Lindi. Mzee Sultani Ungando aliona ajabu sana, baada ya kuuliza khabari za siku nyingi mara moja, mzee Mbawana Nyengo alianza kumhubiria mzee Ungando juu ya umuhimu wa kujiunga katika Jumuiya ya Ahmadiyya. Huyu ni yule, wote wawili walipokuwa kule Lindi alitaka kumrabu fimbo Sheikh Mataka kwa ajili ya kuitanga Ahmadiyya! Mzee Ungando akamuuliza Mzee Mbwana Nyengo vipi anatangaza umuhimu wa kujiunga katika Ahmadiyya! Je, sasa amejiunga nayo? Jibu kutoka kwa mzee Nyengo lilikuwa ndiyo amejiunga tayari. "Si mimii tu bali hata babu yako Mwalimu Rashindi Ungando na wakazi wote wa Nyipara hii wamejiunga katika Ahmadiyya" alisema mzee Nyengo. Naye mzee Sultani Ungando alimthibitishia swahiba wake kwamba hata yeye ameshajiunga mara tu alipofika Dar es Salaam akitokea Lindi.

NDUGU NA JAMAA WALISEMA NINI?

Kabla Mzee Ungando hajajiunga katika Jumuiya ya Ahmadiyya, ndugu, jamaa na marafiki kadhaa walimuona ni mtu wa maana sana anayefaa kati yao kuwa kiongozi. Hiyo ilitokana na kupata eliimu ya Kurani tukufu na hii elimu tuiitayo ya Kizungu. Mzee Ungando alikuwa amepata heshima kubwa na kukubalika katika familia yake na sehemu mbalimbali. Alikuwa mtoto wa Murshid. Alidhikirisha na mengineyo. Katika hali kama hiyo mzee Sultani Ungando akakata kamba na kujiunga katika kundi la Sayyidna Ahmad a.s. Ndugu, jamaa na marafiki zake wengi walishangazwa sana huku wengi wao wakihisi mzee Ungando amepewa kitita cha fedha kujiunga katika Ahmadiyya. Mara kadhaa walituma ujumbe wa watu ili kumshawishi arejee kwenye Usuni.

Wakati fulani ndugu zake mzee Ungando walituma ujumbe wa watu watatu hivi ili wafanye kila liwezekanalo muradi mzee Ungando arudi katika Usuni. Mkuu wa ujumbe huo aliweza kuzungumza na mzee Ungando kwa masiku kadhaa. Siku moja walichukuzana hadi kwa Sheikh Amri Abedi. Huko kwa saa kadhaa walizungumza mambo mbalimbali kuhusu Ahmadiyya. Mwisho wa mazungumzo, mjumbe huyo alijiunga katika Jumuiya ya Ahmadiyya. Allahu Akbar.

Naam, khabari zikarejeshwa kwa waliotuma huo ujumbe kwamba kiongozi mwenyewe wa ujumbe naye amejiunga na Ahmadiyya. Jamaa na ndugu wa mzee Ungando kutoka kule Rufiji wakatuma ujumbe mwingine. Ujumbe huo haukuwa wa watu wala mtu, bali maneno. Waliagiza ile cherehani waliyompa yule mjumbe aliyetangulia na kujiunga katika Ahmadiyya irejeshwe kwao. Ni katika mwaka 1958 haya yanafanyika. Yanakupata lakini?

MTIHANI

Huko nyuma tulikotoka mikutano yetu ya Jumuiya ilikuwa inatembea. Mwaka huu Kigoma, mwaka unaofuata unakuwa mkoa mwingine. Mwaka 1977 mkutano wa Jalsa salana ulifanyika kule Mtama, mkoa wa Lindi. Wanajumuiya wengi kutoka Dar es salaam walielekea huko kwa ajili ya kuhudhuria Jalsa hiyo, mmoja akiwa mzee Sultani Ungando. Msafara ulitoka Dar kuelekea Lindi kwa gari maalum la kukodi. Gari hilo lilipofika kijiji cha Chumbi-Muhoro, mzee Ungando akapata khabari kwamba kakaye yu pale na haliye ni mbaya sana. Mzee Ungando alimtaarifu sheikh Jamil ambaye ndiye alikuwa Mbashiri Mkuu wa miaka hiyo na Kiongozi wa msafara huo. Sheikh Jamil alimruhusu mzee Ungando ashuke na abaki pale kuangalia hali ya huyo mgonjwa. Mzee Ungando alibaki pale na msafara ukaendelea kwenda Mtama Lindi.

Mzee Ali Mohammed Ungando ambaye ndiye kaka wa mzee Sultani aliaga dunia baada ya wiki moja. *Inaa Lillahi wainaa Ilaihi Raajiuun*. Kijiji pale Chumbi palikuwa hakuna Ahmadiyya hata mmoja, mzee Sultani Ungando akachanganyikiwa atazikazikaje! Alijikaza na kupeleka maombi kwa Allah Amsaidie katika hilo kwa kumuonyesha njia ya kufanya.

Mzee Sultani Ungando alimwambia sheikh wa kijiji cha Chumbi kukosha mwili wa marehemu bila ya kumkamua ngama. Yule sheikh wa Kisuni akajibu kwa kusema k wamba yeye atafanya kama alivyofundishwa na masheikh wake wala yeye si mwanafunzi wa mzee Ungando. Akasusa sheikh yule kuosha maiti huyo.

Mzee Sultani akapata ujasiri wa ajabu sana. Pekee akauosha mwili wa kaka yake na kuuvisha sanda. Hata swala ya jeneza aliswali peke yake. Kwa haya baadae tena, watu wengine watatu walijiunga naye na huku kundi kubwa wakiangalia tu kwa macho. Lakini katika wakati wa kwenda kuumzika marehemu watu wengi walishiriiki kuchimba kaburi na kuzika, kwa maana ya kufukia kaburi.

MABADILIKO MAKUBWA

Mimi mwandishi wa khabari hizi, wakati nazungumza na mzee Ungando mnamo mwaka huo 2007 kwenye mazungumzo maalum, aliniambia kwamba yeye alipojiunga tu katika Ahmadiyya, mabadiliko mengi sana yalijitokeza. Ya maisha ya hapa duniani na kiroho. Kwa mfano akanieleza. Pale alipokuwa anafanya kazi kule *Cooper Motors Company Limited*, bosi wake ambaye aliweza kupunguza mshahara wake kwa shilingi 50 tu, baadaye kampuni ilimfukuza kazi kwa kosa la kuiba kopo moja tu rangi. Baada ya miezi mitatu bwana mkubwa huyo aliaga dunia!

Jumuiya ya Ahmadiyya ilitoa vikaratasi au niseme vipeperushi vyenye anuwani ya maneno "UKADIANI NI NINI?" Ndani ya vipeperushi hivyo, Sheikh Kaluta Amri Abedi alinukuu kauli ya Seyidna Ahmad a.s. kwamba Mwenyezi Mungu anazungumza na waja wake wapenzi hadi hivi leo. "Hivi sasa" vipeperushi hivyo viliandikwa "Mwenyezi Mungu Anazungumza na Khalifa mtukufu wa Pili wa Seyidna Ahmad a.s.. Yeyote mwenye matatizo yanayomsibu anaweza kumwandikia ili amuombee kwa Allah".

Wakati huo, mzee Ungando tayari ameshazawiji wala alikuwa bado hajajaaliwa kupata mtoto. Maandiko

Endelea uk. 10

Mzee Sultan Ungando

Kutoka uk. 9

aliyoyasoma kwenye kipeperushi hiki yalimsukuma mzee Ungando kusonga mbele. Basi akaandika barua ya maombi akimwambia Khalifa Mtukufu wa Pili kwamba amuombee kwa Mwenyezi Mungu apate mtoto. Wakati anatuma barua ya maombi hayo, mke wake aliye naye ameshakaa naye miaka minne bila dalili ya mkewe huyo kupata mimba.

Haukupita muda mrefu majibu ya barua ya mzee Ungando yakarudi. Majibu yalimwambia kwamba maombi yamefanyika na Inshallah atapata alichoomba. Ni kweli mnamo tarehe 12 Oktoba, mwaka 1961 mzee Ungando alijaaliwa kupata mtoto wa kike ambaye alipewa jina la Mariyam.

Pakapita miaka kumi bila kupata mtoto mwingine. Ulifikia wakati Mariyam alimuuliza mzee Ungando kwa maneno "Baba, mimi nitapata ndugu yangu?" Mzee Sultani Ungando alimjibu binti yake huyo kwamba Mwenyezi Mungu Akipenda itakuwa hivyo.

Hata hivyo, mzee Ungando aliniambia kwamba swali la bintiye lilimsukuma kwa mara ya pili kuandika tena barua kwa Khalifa mtukufu, lakini sasa Khalifa wa Tatu. Alimweleza tukio lote la khabari hii jinsi lilivyojiri, kwa hiyo akamtaka Khalifa wa tatu naye amuombee apate wana zaidi. Majibu kutoka kwa Khalifa wa tatu yaliletwa , nayo yalikuwa yanaeleza kwamba maombi yamefanyika na Inshallah mzee Ungando atapata anachokiomba.

Ni kweli, ni kweli tupu. Mnamo mwaka 1972, mzee Ungando alipata mtoto wa kike aliyepewa jina la Bushra. Mwaka 1974, akapatikana Bashir na mnamo mwaka 1980 akapatikana mtoto wa kiume aliyepewa jina la Imamu.

CHANZO CHA JAMAAT KUPATA ENEO KITONGA

Baadhi ya wanajumuiya walitupa macho yao mbali. Hawakuona kitu ila giza totoro. Hao walikuwa wanafikiria maendeleo ya baadaye ya Jumuiya. Walidhani ni jambo jema sana kama Jumuiya itakuwa na kituo chake kitakachokuwa na shule, hospitali, Jalsa Gah na vitu vingine. Miongoni mwa wanajumuiya waliokuwa na mawazo hayo ni Amir wa zamani aliyekwisha tangulia mzee Ali Saidi Mosse.

Mzee Mosse - akiwa Amir wa Jamaat ya Tanzania - aliitisha kikao ambacho aliwaalika wadau hao wa maendeleo na kuwaomba watafakari juu ya njia ya kuchukua ili kutimiza azma hiyo. Ni katika kikao hicho ambapo watu kadhaa waliahidi michango yao ya aina mbalimbali, mzee Sultan Ungando bila kupepesa macho wala kufikiria sana, yeye akasema atatoa sehemu ya shamba lake lililoko kijiji cha Kitonga ili Jumuiyya itumie sehemu hiyo kwa mambo mbalimbali. Hicho kimekuwa ni chanzo kikubwa sana cha kituo chetu cha Kitonga. Hivi leo Kitonga ndio hiyo.

Kwa ufupi sana huyo ndiye Mzee Sultani Mohammed Ungando ambaye hivi sasa hatunaye tena hapa duniani. Yake japokuwa nimeyawakilisha kwenu kwa uchache, lakini mimi naona hata hiki kidogo ndani yake limo somo. Tunalo la kujifunza kutoka kwa ndugu yetu huyu. Basi si vibaya bali ni vyema zaidi wewe na mimi tukaanza kujifunza kuanzia sasa.

ALLAH MWINGIZE PEPONI.

Msiba ulotujia, ni mtihani mangungu
Jamaa na familia, nyoyoni tuna utungu
Tupe subira Jalia, tusiwe pindu pindingu
Allah, Mwingize peponi, al-akhi mahabubu.

Binafusi ninalia, namlilia mwenzangu
Mwenzangu katangulia, ziko ngapi siku zangu?
Chache najitabiria, itafika zamu yangu
Allah, Mwingize peponi, al-akhi mahabubu.

Ni wewe Mola Samia, kwenye ardhi na mbingu
Na vilivyomo jamia, Mmiliki Wewe Mungu
Chote kinachotukia, Kwako hakina ukungu
Allah, Mwingize peponi, al-akhi mahabubu.

Kama ali na khatia, kidogo au la chungu
Tafadhali nagutia, Usimkung'ute rungu
Samehe na kumtia, kwenye janati ya tangu
Allah, Mwingize peponi, al-akhi mahabubu.

Na kama alikosea, kwenye huu ulimwengu
Nduguze twamuombea, Mghufiri ewe Mungu
Firdausi akae, aketi bila ya zungu
Allah, Mwingize peponi, al-akhi mahabubu.

Muhenga Al-Ustadhi Khamisi Wamwera

Kimbangulile – Mbagala Rangi Tatu – Dar es salaam.

ASEMAVYO MASIHI ALIYEHIDIWA

ULEZI BARABARA WA WATOTO

Ninaamini ya kwamba kupiga watoto katika namna ambayo mpiga watoto aliyekubuhu hujifanya kuwa mshirika wa Allah katika kuwaongoza na kuwafunza watoto ni aina ya USHIRIKINA.

WAOMBEENI WATOTO BADALA YA KUWAADHIBU

Mtu mwenye ghadhabu kali anapochokozwa na kumuadhibu mtoto, huchukua nafasi ya adui kutoa hasira zake na hutoa adhabu kali sana kuliko kosa lililofanywa. Mtu mwenye kujiheshimu na anayejidhibiti, ambaye pia ni msamehevu na mwenye kujiheshimu, ana haki ya kumsahihisha mtoto hadi kiasi kile tukio husika linavyohitajia au atafute namna ya kumuongoza mtoto. Lakini mtu wa ghadhabu na kichwa ngumu ambaye hutibuliwa kirahisi hafai kuwa mlezi wa watoto. Natamani ya kwamba, badala ya kuadhibu watoto, wazazi wayaelekee maombi, na waifanye kuwa tabia kuwaombea watoto wao kwa moyo wa dhati sana; kwani maombi ya wazazi kwa ajili ya watoto wao hukutana na ukubali maalum.

Kisa Chenye Mafunzo makubwa

Kisa cha kichekesho kimesambazwa na gazeti la 'Al-hayat kinasema juu ya Muingereza mmoja mwenye asili ya Kiasia anaeishi katika mji wa Yorkshire Uingereza. Anaeleza kwamba nimedhikika na kuchoshwa sana kwa nyumba yangu kuingiliwa na wezi mara kwa mara katika mji huu maarufu kwa ujambazi. Nilipochoshwa na jambo hilo nikaondosha mtambo wa alarm 'indhar' wa kujulisha anapokuja mwizi. Na nikatoka kwenye jumuiya ya majirani ya ulinzi shirikishi wa majumba. Nikasimamisha bima ambayo ilikuwa inapanda malipo yake kila nikiripoti matukio ya wizi nyumbani kwangu. Nikawa sihisi amani tena. Badala ya yote hayo, nilinyanyua na kupachika bendera nyeusi juu ya nyumba yangu iliyoandikwa لَآ إِلَٰهَ إِلَّا ٱللَّهُ مُحَمَّدٌ رَّسُولُ ٱللَّهِ. Yaliyotokea baada ya hapo polisi wa eneo zima la Yorkshire, Baraza la amani la England na Scotland Yard na vikosi vya mashushu na upelelezi vya MI5, MI6, na CIA na vyombo vyote vya ulinzi na usalama vya Uropa wakawa wanaichunga nyumba yangu masaa 24 kwa mwaka mzima. Hata watoto wangu wanafuatwa wanapokwenda skuli na kurudi. Na mke wangu haendi sokoni illa huzungukwa na wapelelezi wa siri na wadhahiri. Na mimi siendi kazini kwangu ila hufuatwa na askari wa siri. Na nyumba yangu ilikuwa ikilindwa na magari ya polisi wakibadilishana doria usiku na mchana kwa masaa 24. Hakuna mtu aliyethubutu tena kuikaribia nyumba yangu kwa wizi au uhalifu wowote. Na sijawahi kuhisi amani kama hiyo katika maisha yangu yote kamwe....```

Nabii Isa wa Nazareti (a.s.) alikufa tangu kale

Kutoka uk. 12

kwa njia ya mabadiliko ya kimaumbile, imeelezewa hapa kimuhtasari. Sawa na aya hii inaonekana kwamba pana hatua tano ambazo mwanadamu hupitishiwa kimaumbile, katika safari yake hii asiyokuwa na hiyari nayo.

Kwanza kabisa, mwanadamu hupitishiwa kwenye ulimwengu wa madini, bali hufanywa kuwa ni sehemu ya ulimwengu huo. Kisha hupitishiwa katika ulimwengu wa mimea huku akiwa ni sehemu ya ulimwengu huo. Kisha kisha hupitishiwa katika ulimwengu wa miili ya wazazi akifanywa kuwa ni sehemu ya ulimwengu huo. Tofauti kabisa na hali yake katika hatua mbili zilizotangulia ambapo hali ya uzima na ubinadamu wake hazikuwa zikijidhihirisha kinagaubaga, kwenye hatua hii ya tatu mabadiliko makubwa zaidi hutokea kwani uzima wake na ubinadamu wake huanza kujidhihirisha kwa uwazi – naam, katika tumbo la uzazi. Inaonekana ni kwa sababu ya umuhimu wa hatua hii ambapo "msafiri huyu", mwanadamu huhitimisha hali yake ya kuwa yu kama 'mfu' na kuhuishwa kufanywa mzima, ndipo hekima ya Allah ikatoa tafsiri ya hatua hii kwa kusema: "Kisha Tukaumba mbegu kuwa pande la damu, na Tukaumba pande la damu kuwa pande la nyama, kisha Tukaumba pande la nyama kuwa mifupa, na mifupa Tukaivika nyama, kisha Tukaifanya kuwa kiumbe kingine. Basi Mwenye Mibaraka ni Mwenyezi Mungu Mbora wa Waumbao" (23:15). Kisha baada ya kuzaliwa, mwanadamu hupitishiwa kwenye hatua ya mautiakaingizwa kwenye dunia ya pili amabayo katika dini ya Kiislamu huitwa "Barzakh". Kisha huhuishwa na kufikishwa mbele ya Mola wake, Mbora wa Mahakimu.

Sasa, tukirejelea habari za Nabii Isa bin Maryamu wa Nazareti (a.s.) ni sharti tukumbuke ya kuwa safari ya 'mbele-kwa-mbele' ya mwanadamu kurudi kwa Mola wake ndiyo iliyomfikisha yeye hapa duniani sambamba na wanadamu wengine wote, na ambayo bila ya hiari yake, ilimtoa kutoka humu duniani kwa kumfikishia hatua ya mauti tuliyoitaja hapo juu, na kumuingiza kwenye dunia ya Barzakh kwenda kutekeleza hatua ya mwisho ya safari hii ya kuhuishwa tena na kurudishwa kwa Mola wake. Wale wanaompenda Isa bin Maryam wa Nazareti (a.s.) kiasi hiki kwamba hawako tayari kumnasibishia mauti, hivyo basi hawana budi kuelewa ya kuwa kadri mwanadamu anavyohusika, safari hii ambayo Qur'an Tukufu imetupatia muhtasari wa hatua zake, ndiyo maumbile yenyewe na hapana hatua yake hata moja inayoweza kuepukika au kurudishwa kinyumenyume baada ya kuwa imetimilizwa. Haiwezekani hata kidogo kwa mwanadamu kurudi ndani ya tumbo la uzazi baada ya kuhuishwa humo na kuzaliwa. Na ndivyo isivyowezekana kwa wafu kurudi tena humu duniani baada ya kufikishwa kwenye hatua ya kifo na kuingizwa kwenye dunia ya pili ya Barzakh. Hii ndio hali ya wafile wote akiwemo Nabii Isa bin Maryamu wa Nazaret (a.s.).

Na kwale wale ndugu ambao licha ya maelezo haya ya safari ya mwanadamu ya kimaumbile ya kurudi kwa Mola wake isiyoweza kuepuka hatua ya kifo, bado nyoyo zao hazikubali kifo chake, basi hao sawa na hali zao za kiroho Mwenyezi Mungu Amewapatia dalili mbalimbali katika Qur'an Tukufu za kuthibitisha kifo cha Nabii huyu wa wana wa Israeli (a.s.). hapa sisi tutawakariria aya moja ya dalili hizo inayotekeleza pakubwa shabaha ya mada tunayoizungumzia. Kwanza kabisa, Mwenyezi Mungu Anatuthibitishia ya kuwa Nabii Isa au Yesu (a.s.) na mamake wanaabudiwa na Wakristo kama miungu wawili badala ya Allah: siku ya hukumu Mwenyezi Mungu Amemwekea Nabii bin Maryam swali hili: "Ewe Isa bin Maryamu! Je wewe uliwaambia watu; nishikeni mimi na mama yangu kuwa waungu wawili badala ya Mwenyezi Mungu? (5:117) na pia (Wakristo) wamewafanya wanazuoni wao na watawa wao kuwa ni miungu badala ya Mwenyezi Mungu na Masihi mwana wa Maryam pia (9:31). Pili, Mwenyezi Mungu Ajuaye ghaibu, Anatujulisha hali halisi ya wale wanaoabudiwa na wafuasi wao badala ya Mwenyezi Mungu hawaumbi chochote, bali wao wameumbwa: ni wafu si wazima, na hawajui watafufuliwa lini (16:13-14). Aya ya Qur'an Tukufu inadokezea kuwepo kwa kanuni ya Allah ya kuwa hapana anayeweza kuabudiwa na wafuasi wake na akaendelea kuwa hai. Ni kazi bure hivyo basi, kuendelea kuwaabudu waja wa Mungu kama vile Yesu au Isa bin Maryam wa Nazareti, Budha, Krishna n.k., kwani hao wote ni wafile na hawajui watafufuliwa lini. Huruma na mapenzi yetu juu yao vitabakia palepale, lakini haiwezekani kabisa kubatilisha kanuni ya Allah kwamba wao wote ni wafu.

Na neno letu la mwisho ni kwamba sifa zote njema zinamhusu Allah, Mwenye Kuhuisha, Mwenye Kufisha, Mbora wa Waumbao na Mola wa Walimwengu.

Kiini Cha Maombi ya Ikhlasi.

Kutoka uk. 12

maombi yake yanakubaliwa.

Masihi Aliyeahidiwa (as) anasema, 'Maombi yana athari ya kiusumaku kwa kuwa yanavuta neema na baraka [za Mungu].'

Masihi Aliyeahidiwa (as) anasema, 'Tunasema kwamba yule, ambaye hujiweka mbele ya Mungu Mwenyezi ... na anaangalia mipaka na amri zake kwa heshima kubwa .... ambaye anajisahihisha mwenyewe na matokeo yake anaheshimu adhama Yake. Masihi Aliyeahidiwa (as) anasema, 'Mtu huyo atakuwa na haki ya kupata baraka za Mungu.

Jumuiya yetu lazima isali sala ya Tahajjud (sala ya nafali kabla ya alfajiri) lazima juu yao wenyewe, hata kama Rakaa mbili tu, kwa kuwa angalau kupata nafasi ya kuomba. Masihi Aliyeahidiwa (as) anasema, "Maombi ya wakati huo yana athari ya kipekee (yaani wakati wa Tahajjud), kama huombwa kwa huzuni ya kweli na shauku."

Masihi Aliyeahidiwa (as) anasema: 'Kuna jambo lingine ambalo ni muhimu kwa Jamaat yetu kulishika, ambalo ni kwamba wanajamaat wanapaswa kujiepusha kutoa maneno yasiyo ya maana na vitu visivyofaa (weka ulimi wako utakasike dhidi ya kutoa kauli za kipuuzi). Usiumize hisia ya mtu yeyote na wala usieleze kitu chochote kisichofaa au kibaya. 'Masihi Aliyeahidiwa (as) anasema: Ulimi ni mlango wa uhai wetu na kutakasa ndimi zetu humleta Mungu Mwenyezi kuja kwa mlango wetu.

Masihi Aliyeahidiwa (as) anasema: 'Unapaswa kutenda juu ya hili kama ilivyosemwa kuwa: "Wewe tu tunakuabudu na Wewe tu tunakuomba msaada." Hata hivyo, kumbuka kwamba usafi wa kweli hukaa katika kile kilichosemwa kuwa: "Yule tu kikweli amefaulu ambaye huitakasa (nafsi yake)." Kila mtu ajue kuwa ni wajibu wake kujirekebisha mwenyewe. "Masihi Aliyeahidiwa a.s anasema: 'Wanaoweza kutumaini neema ya Allah ni wale tu ambao hawaachi kamwe kusali, kuomba msamaha kutoka kwa Allah kutokana na dhambi zao na kutubu na kujizuia kufanya makosa.

Masihi Aliyeahidiwa (as) anasema: 'Dhambi ni sumu ambayo huangamiza mtu na husababisha adhabu ya Kimbingu. Dhambi huondoa hofu na upendo wa Allah Mwenyezi ndani ya moyo wa mtu (Masihi Aliyeahidiwa a.s anaelezea kwamba mtu anaweza tu kuacha dhambi ikiwa atashikamana na Allah kwa upendo na hofu na atajua kwamba Allah Humuona wakati wote).

Akielezea maana hasa ya sala, Masihi Aliyeahidiwa (a.s) anasema: Kuna aina mbili za sala. Ya kwanza ni sala ya kawaida (maombi ya kawaida yanayofanywa na mtu) na pili ni pale mtu anapoinua sala yake kufikia kileleni. Hiyo ndio aina hasa ya sala (wakati mtu anapokuwa na hali ya mahangaiko katika sala na inafikia kileleni). ' Masihi Aliyeahidiwa (a.s) anasema: "Ni lazima kwa mtu kuendelea kusali hata kama hana shida au matatizo yoyote. Wakati mwingine, mitihani na matatizo yanamzingira mtu kwa namna ambayo anakuwa hana hata fursa ya kusali." Hivyo, kama mtu atasali kabla, sala hizo zitampa faida hapo baadae katika nyakati za aina hiyo.

Kisha Masihi Aliyeahidiwa (a.s) anaelezea kwamba Qur'ani inaanza kwa dua na inaishia kwa dua na anasema: 'Allah Mwenyezi anaianza na kuimaliza Qur'ani Tukufu kwa dua. Sura Faatiha ni dua na Sura Al-Nas pia ni dua. Hii ina maana kwamba binadamu ni dhaifu na bila Baraka za Allah kamwe hawezi kuhalisika. Mpaka pale mtu anapopokea msaada na muawana wa Allah hawezi kupata maendeleo ya Taqwa. Ni wale tu ambao Mungu Mwenyezi Amewapa baraka Zake ndio ambao wanaepushwa na mvuto wa dunia hii. Lakini, mtu azingatie kwamba Baraka za Mungu Mwenyezi zinaanza na maombi hivyo mtu ni lazima pia aliombee hilo.

Akiwa anaelezea sifa za waaminio, Masihi Aliyeahidiwa (a.s) anasema kwamba imesemwa bayana ndani ya Kuruani Tukufu 'Hakika, wamefaulu waaminio, ambao ni wanyenyekevu katika Sala zao,' (23:2-3). Hii ndio kusema kwamba ni wale waaminio wanaoonyesha unyenyekevu katika sala zao ndio wanaofaulu. Wanajitupa kwa unyenyekevu wa hali ya juu kabisa na upole na wanajawa na hali ya kushindwa. Ni hapo tu ndipo mlango wa mafanikio unafunguliwa kwa ajili yao ambao kupitia huo pendo la dunia linapungua, kwani aina mbili za penzi haziwezi kukaa sehemu moja. Masihi Aliyeahidiwa (a.s) anaandika: Hiyo ndio kusema mnamuhitaji Mungu na pia mnaihitaji dunia hii ovu, lakini hilo ni wazo tu ambalo haliwezekani kupatikanika na ni upumbavu. Hauwezi kuwa navyo vyote viwili. Bila shaka, kama unamuhitaji Mungu, basi Mungu Anao uwezo wa kukupa baraka za dunia hii; lakini kama unatafuta tu haja za dunia hii, basi huwezi kumpata Mungu.

Maombi yanakubaliwa kama utazifanya haja na tamaa zako ziendane na Anayoyaridhia Mungu Mwenyezi. Akielezea nukta hii Masihi Aliyeahidiwa (a.s) anasema: Mtu ni lazima aipoteze dhati yake ndani ya dhati ya Allah na kwa kuachana na haja na tamaa zote ni lazima ashikilie Matakwa na Amri za Allah na awe chanzo cha Baraka zitakazomjia yeye mwenyewe, watoto wake, mke wake, jamaa na ndugu zake na pia kwangu mimi.' Masihi Aliyeahidiwa (a.s) anasema: Mtu kamwe asiwape wapinzani fursa ya kuleta shutuma. Mungu Mwenyezi Anasema 'Na miongoni mwao kuna baadhi wanaoziua nafsi zao kwa kukandamiza matamanio yao, na miongoni mwao kuna baadhi wanaodumu katika njia iliyonyooka, na miongoni mwao kuna baadhi wanaowashinda wengine katika matendo ya wema' (35:33). Masihi Aliyeahidiwa (a.s) anasema kwamba sifa mbili za kwanza ni za chini, na ni lazima tuwe Saabikuuna bilkhairaat, yaani wale tunaowashinda wengine katika mema.

Sio sifa nzuri kuganda katika sehemu moja. Oneni jinsi gani maji yaliyotuama mwishowe yanavyokuwa machafu na kutokana na kuchanganyikana na matope yanakuwa hayafai yasiyo na ladha. Kwa upande mwingine, maji yatiririkayo daima yanakuwa mazuri, masafi na yanapendeza. Hata kama kuna matope chini yake, yanakuwa hayaathiri maji hayo. Hii ndio hali ya mtu kwamba asibaki ametuama katika sehemu moja. Hali hiyo ni ya hatari. Hivyo, ili maombi yakubaliwe, ni lazima kwamba mtu afanye maendeleo katika kutenda mema kwa kila siku. Katika maendeleo haya endelevu, yanaongoza kwenye mwisho mwema. Kisha Masihi Aliyeahidiwa (a.s) anasema kwamba Mungu Mwenyezi Amefundisha dua ifuatayo katika Kuruani Tukufu. 'Na uifanye mbegu yangu iwe ya ucha Mungu kwangu' (46:16). Wakati mtu anapofanya mabadiliko halisi katika nafsi yake, ni lazima aendelee kuomba kwa ajili ya watoto wake na mke wake kwa sababu mara nyingi mitihani ya mtu inatokana na watoto na mke wake. Hivyo, matatizo mengi ya mtu na shida ni kutokana na watoto na mke. Kwa hiyo, ni lazima tuzingatie kikamilifu mafunzo na kuongoka kwao na tudumu katika kuwaombea.

Katika sehemu moja Masihi Aliyeahidiwa (a.s) anasema: "Imehadithiwa kuhusu mtakatifu mmoja ambaye alikuwa ndani ya merikebu. Kikaja kimbunga baharini na merikebu ikawa karibu kuzama lakini iliokoewa kutokana na dua zake. Akiwa anafanya maombi aliambiwa kwa njia ya wahyi kwamba tumemuokoa kila mtu kwa sababu yako. Lakini, hii haipatikani kwa kutoa maneno matupu tu, mtu ni lazima afanye jitihada kubwa ili kulipata hili. Ushauri wetu ni kuendelea kufanya jitihada kujiweka kuwa mfano mzuri. 'Wanafanya wanachoamrishwa. (16:51). Masihi Aliyeahidiwa (a.s) anatuelekeza kwenye umuhimu wa maombi anaposema 'Wamebarikiwa wafungwa ambao hawachoki katika kufanya maombi, kwani siku moja watakuja achiwa huru. Wamebarikiwa vipofu ambao sio walegevu katika maombi yao, kwani siku moja wataona. Wamebarikiwa wale waliolala kwenye makaburi ambao wanafanya maombi kwa Mungu kwa msaada na auni, kwani siku moja watatolewa makaburini'.

Akitutanabahisha juu ya hili, Masihi Aliyeahidiwa (a.s) anasema: Mmebarikiwa nyie ambao hamchoki katika maombi yenu na nyoyo zenu zinayeyuka mkiwa mnasali, na macho yenu yanatiririsha machozi, na moto unawaka katika vifua vyenu na mnapelekwa katika vyumba vyenye giza na misitu kutafuta upweke, na mnafanywa muwe hamna utulivu, vichaa na mlio zimia, kwa sababu mwishoni mnakuwa ndio wenye kupokea Baraka. Mungu Ambaye Kwake tunawaiteni ni Mwema, Mwenye Baraka, Mpole, Mkweli, Mwenye Imani na Mwenye Huruma kwa wale ambao ni wapole. Nyie pia muwe wenye imani na muombe kwa unyenyekevu kamili na utiifu ili Awabarikini. Jiondoeni kwenye ghasia za dunia na msizifanye imani zenu kuwa jambo la ushindani binafsi. Kubalini kushindwa kwa ajili ya Mungu ili muwe warithi wa ushindi tele iliyo mikubwa mikubwa. Mungu Ataonyesha miujiza kwa wale wanaofanya maombi na Atawapa upendeleo usio wa kawaida kwa wale wanaoomba. Dua inatoka kwa Mungu na inarudi Kwake'

Masihi Aliyeahidiwa (a.s) anawaonya wanajumuiya: 'Kama mtu anaishi maisha yaleyale yasiyo matakatifu na machafu kama alivyokuwa kabla ya kufanya baiati na pia yule anayejihesabu kuwa yumo katika Jumuiya na anaonyesha mfano mbaya, na anaonyesha udhaifu katika khulka zake na imani, basi mtu wa aina hiyo ana hatia ya kufanya udhalimu wa hali ya juu. Hii ni kwa sababu anadhalilisha jina la Jamaat na pia anawapa wengine fursa ya kuninyooshea kidole. Watu wanachukia mfano mbaya wakati mfano mzuri kabisa huwa unawahamasisha wengine.

Masihi Aliyeahidiwa (a.s) anaendelea kusema: Leo na kesho ya mtu isiwe sawa. Kama leo na kesho ya mtu inakuwa sawa katika maendeleo ya taqwa, basi mtu wa aina hiyo atakumbana na hilikisho. Lakini, kama mtu anaamini Mungu na ana imani naye kamili basi kamwe hata hilikishwa, kwa kweli kwa sababu yake pekee malaki ya roho zinaokolewa.' Mfano wa hili ulitolewa ambapo Mungu Mwenyezi alimuokoa kila mtu katika merikebu kutokana na kuwepo kwa mtakatifu mmoja. Hivyo, Mungu Mwenyezi Anawaangalia sana watumishi Wake.

Masihi Aliyeahidiwa (a.s) anasema: 'Silaha yetu ni maombi; ni lazima tulenge kwenye maombi. Kazi zote tunazotaka kuzifanikisha zinaweza kufanikiwa tu kwa maombi. Maombi yana nguvu nyingi'

Masihi Aliyeahidiwa (a.s) zaidi anasema: 'Inasimuliwa kwamba siku moja Mfalme fulani alitoka kwenda kuishambulia nchi fulani. Njiani, mtu mmoja masikini akapokonya hatamu za farasi... (hiki ni kisa) na akasema kwamba kama utaacha kuendelea mbele sitapigana dhidi yako.' Mfalme akashangazwa sana na hilo na akauliza: 'Wewe ni ombaomba tu, masikini na hauna chochote. Unawezaje kupigana na mimi? Akajibu: 'Nitafanya vita na wewe kwa kutumia silaha ya maombi ambayo nitayafanya karibukaribu na alfajiri' yaani katika maombi yanayofanyika kwenye sala ya Tahajjud. Mfalme akajibu: 'Siwezi kupigana dhidi ya hilo' na akarudi. Hivyo, hii ndio nguvu ya maombi na ndiyo ambayo Masihi Aliyeahidiwa (a.s) aliyoielezea.

Masihi Aliyeahidiwa (a.s) anaendelea kwa kusema: 'Kwa kifupi, imeshakadiriwa na Mungu Mwenyezi kwamba maombi yanatoa nguvu kubwa. Mungu Mwenyezi Amenifahamisha kwa kurudiarudia kwa kupitia wahyi kwamba kila kitu kitatokea kwa msaada wa maombi. Silaha yetu ni maombi na sina silaha nyingine minghairi ya maombi. Maombi yetu yanapofikia kilele chake, adui anashindwa yeye mwenyewe.' Hivyo, swala hili ambalo limetajwa na Masihi Aliyeahidiwa (a.s) ni la muhimu sana na ni lazima lieleweke, kwamba kama maombi yetu yatafikia kiwango fulani, ambacho mfano wake unatakiwa kwetu na Mungu Mwenyezi, maadui zetu wataangamizwa. Masihi Aliyeahidiwa (a.s) anasema: 'Kwa maoni yetu, hakuna silaha bora zaidi ya maombi. Ni mwenye bahati yule anayeuelewa ukweli huu ambao kwa njia yake Mungu Mwenyezi sasa Anataka kuipa dini maendeleo."

Mwishoni kuna dua ambayo Masihi Aliyeahidiwa (a.s) aliiomba kwa ajili ya Umma wa Kiislamu na pia kwa ndugu zetu wasio Waahmadiyya kwa ujumla. Masihi Aliyeahidiwa (a.s) anasema: 'Ee Mola wangu! Pokea dua yangu kuhusu watu wangu na kwa maumivu yangu makali ya moyo na ari ninapofanya maombi kwa ajili ya ndugu zangu. Ninakuomba kwa kupitia kwa Muhuri wa Manabii, muombezi wa wenye dhambi, ambao uombezi wake unakubaliwa. Ee Mola wangu! Waondoe kwenye giza na walete kwenye nuru yako. Walete kutoka mbali waliko wafike karibu yako. Ee Mola wangu! Wabariki wale wanaonilaani na wanafanya jitihada kunizuia. Waepushe watu hawa na hilikisho na ingiza muongozo wako kwenye mioyo yao. Usitizame makosa yao na madhambi na wasamehe. Wape ulinzi, Waongoze na Watakase. Wape macho yatakayowawezesha kuona, Wape masikio yale ambayo yatawawezesha kusikia, Wape mioyo ambayo kwayo wanaweza kuelewa na mnunurisho ule utakaowawezesha kuelewa (ukweli). Wape baraka na wasamehe kwa wanayoyasema, kwani hao ni watu wasio jua kitu. Ee Mola wangu! Ninaomba) kwa minajili ya Muhammad Mustafa (saw) na heshima yake ya juu, ambapo angetumia mausiku mengi akisujudu na mchana katika uwanja wa vita, na pia kwa sababu ya wale askari farasi ambao wangeendesha kwa kasi wakati wa usiku na pia zile safari zilizofanywa kwenye mama ya miji yote, na zikawa ndio njia ya mapatano kati yetu na binadamu wenzetu. Fungua macho yao na Uiangazie mioyo yao. Wawezeshe kuelewa sheria za Mungu ambazo umenieleza. Waonyeshe njia ya Taqwa na samehe yale yote yaliyopita. Dua yetu ya mwisho ni kwamba kila sifa njema inamhusu Mungu Mwenyezi, Mola wa Mbingu za juu."

Ninamuomba Allah Mwenyezi Afungue macho ya Umma wa Kiislamu ili wajiepushe na kumpinga aliyeteuliwa na Mungu Mmoja, na baadala yake wawe ni wasaidizi wa Masihi Aliyeahidiwa (a.s). Ninamuomba Allah Atuwezeshe sisi kuwa wale wanaotimiza haki ya maombi. Wale ambao wamehudhuria katika Jalsa ya Qadian ni lazima wazingatie hili mahsusi na ushiriki wao kwenye Jalsa uwe ndio njia ya mabadiliko ya kimapinduzi katika nafsi zao. Ninamuomba Allah Mwenyezi Atuwezeshe sisi sote kufanya hivyo. Amin.

The First Muslim Newspaper in Kiswahili Language since 1936

MapenziyaMungu

Rab. II - Jum. I 1439 AH | JANUARI 2018 | Sulhu 1397 HS

Kutoka Hadithi za Mtume Mtukufu s.a.w

Imesimuliwa na Hadhrat Jabir r.a. kwamba Mjumbe wa Allah s.a.w. alisema: Mfano wa sala tano ni kama mfano wa mto uliojaa maji unaopitia mlangoni na mmoja wenu, naye anaoga humo kila siku mara tano. (*Muslim*).

Kiini cha Maombi ya Ikhlasi.

Na Mwandishi Wetu, Dares Salaam

muhtasari wa Hotuba ya Ijumaa iliyotolewa na - Katika hotuba ya Sala ya Ijumaa ya tarehe 29/12/2017, Kiongozi wa Waaminio, Hadhrat Amir-ul Muminiin - Khalifatul Masih atba alizungumzia juu ya Kiini Cha Maombi ya Ikhlasi.

Baada ya Tashahhud, Taa'udh na Surat Fatihah Hadhrat Amir-ul Muminiin (atba) alisema:

Leo, kwa fadhila za Allah Mwenyezi, Jalsa Salana [Mkutano wa Mwaka] wa Qadian umeanza. Ombeni kwa Allah Mwenyezi kuwa siku tatu za Jalsa huko, zihitimishwe salama na wanajamaat waaminifu wa Jumuiya waweze kufikia malengo ambayo wamejiwekea wenyewe kwa kuja kwenye Jalsa hii.

Lengo hilo ni kumwomba Allah Mwenyezi (kwa ajili ya mtu binafsi, kwa ajili ya maendeleo ya Jumuiya na kushindwa kwa maadui wa Jumuiya), kujitahidi kuboresha hali ya maarifa yetu na hali ya tabia za vitendo vyetu, ili kuimarisha Uhusiano wetu na Allah Mwenyezi na kupata faida kutoka kwayo na kutoka kwenye hali ya kiroho.

Vivyo hivyo, pia ni lazima kuombea ulimwengu wa Kiislamu, ambao baadhi yao wanafanya maovu kwa jina la Allah Mwenyezi na Kiongozi wetu, Mtukufu Mtume Muhammad (saw). Kutokana na uovu kama huo, madai yanaibuliwa dhidi ya Uislamu na Mtume (saw) katika ulimwengu usio wa Kiislamu. Tunapaswa pia kukumbuka kuomba kwa ajili ya (utimilifu wa) lengo, ambalo Masihi Aliyeahidiwa (a.s) alitumwa kwalo; Lengo hilo ni kuwaongoza Waislamu, pamoja na kuwafanya wasio Waislamu wafahamu ukweli wa Uislamu na kuwaingiza katika boma la Uislamu kwa kuwathibitishia ubora wake na kuwavuta.

Vivyo hivyo, tunapaswa pia kuomba kwa hali ya jumla ya ulimwengu wote. Tuombe Allah atoe hekima kwa wanadamu wote, ili waweze kuokolewa kutoka shimo la maangamizo. Leo, ulimwengu unahitaji mahitaji makubwa ya Maombi ya wafuasi wa Masihi Aliyeahidiwa (as). Tunapaswa kuomba kwamba Allah Mwenyezi Aupatie hekima ulimwengu.

Aupatie hekima Ummah wa Kiislamu na watu hawa waweze kuelewa ukweli huu kwamba bila kumwamini yule aliyetumwa na Allah Mwenyezi, hawataweza kudumu, wala kupata wokovu. Naomba waingie mwaka mpya wakiwa wameelewa hili. Naomba Allah Afanye kwamba wapate ufahamu wao.

Leo, nitawasilisha baadhi ya nukuu chache za Masihi Aliyeahidiwa (as) kuhusu falsafa, mbinu na adabu za maombi.

Akielezea kipengele cha msingi na kitovu cha kukubalika kwa maombi, Masihi Aliyeahidiwa (a.s) anasema:

"Bila ya moyo kuwa safi, maombi hayakubaliki. Ikiwa moyo wako umejawa na kinyongo juu ya mtu hata kama kuhusiana na jambo fulani la kidunia, maombi yako hayawezi kukubaliwa. Kwa hivyo, ni muhimu sana kwa kukubalika kwa maombi, kila chuki za kibinafsi na uovu uachwe na maombi ya khushui yafanyike ili kutafuta msaada wa Allah Mwenyezi ili kupata utakaso wa kudumu wa moyo.

Wakati mtu ana huzuni na akapiga magoti mbele ya Allah Mwenyezi katika hali ya udhaifu na kumwomba yeye, basi Allah Mwenyezi huja kwa msaada wake. Hivyo, kanuni hii inapaswa kukumbukwa kila wakati. Ili kupata hali ya huzuni na unyonge katika maombi, ambayo ni sharti la msingi kwa kukubalika kwa maombi, Masihi Aliyeahidiwa a.s alielezea kuwa ni muhimu kutakasa moyo wa mtu kutokana na uovu. Masihi Aliyeahidiwa (as) anasema zaidi, 'Huzuni ni hali ya kukubaliwa kwa maombi.' Sharti la kwanza ni kusafisha mioyo na hali ya pili ni Huzuni. "Kama Mungu asemavyo, (27:63) Kuwa ni,`Au ni nani Anayemjibu aliyedhikika amwombapo na kuondoa dhiki.`

Hivyo, Huzuni ni muhimu kwa maombi na ni muhimu pia kuwa na imani imara katika ukweli kwamba ni Uwepo tu wa Allah Mwenyezi, Ambaye Anayeweza kukusaidia katika hali hii ya dhiki na unyonge. Ni yeye tu, Ambaye anajibu maombi na Huwasaidia watumishi Wake.

Kwa hiyo, leo ninazungumza na Waahmadiyya wa huko Qadian na Jumuiya nzima inapaswa kuzingatia hili, tumia muda wako mwingi katika maombi na katika kumkumbuka Mungu. Mnapaswa kuinama mbele ya Allah Mwenyezi, ili kwamba Allah Mwenyezi, kupitia neema Yake, Aweze kuboresha hali ya Waahmadiyya popote wanapokabiliana na magumu na ili athibitishe wapinzani kutofanikiwa.

Akielezea hali ya dhiki na uhalisia wa maombi, Masihi Aliyeahidiwa (a.s) anasema mahali fulani, 'Usiamini kwamba maombi ni kutamka maneno matupu tu. La hasha, bali maombi ni aina ya kifo, baada ya mtu kupata maisha [mapya], kama tunavyosoma katika mistari ya shairi la Kipanjabi, kuwa, hali ya mtu anayeomba ni kama amekufa na amepoteza kila kitu. Yeye hutokwa kabisa na nafsi yake, ubinafsi wake na maangamizo yote kuwa kwake na hujiweka mwenyewe mbele ya Allah Mwenyezi, katika hali hiyo, basi

Endelea uk. 11

Naam, Nabii Isa wa Nazareti (a.s.) alikufa tangu kale - Quran Tukufu

Kutoka Maktaba Yetu

Miongoni mwa kanuni za kimaumbile asizozipenda mwanadamu, bali na hata kuziogopa sana, ni mauti na kifo. Hawezi mwanadamu akafanya mapatano ya aina yoyote ile na kifo. Habari zozote za kifo, hususan cha yule anayempenda, humjaza huzuni tele. Inaonekana kuwa ni hali ya kimaumbile ya moyo wa mwanadamu kuhunishwa na kifo cha mpendwa hata yule aliyefariki miaka mingi iliyopita. Jambo hili linazidi kudhihirika zaidi katika ulimwengu wa dini ambapo vifo vya Manabii vilivyotokea vizazi vingi vilivyopita, bado vinaendelea kuadhiri roho za waumini wengi hadi hivi sasa. Roho zinatamani laiti Vipenzi hao wa Allah wangelikua hai nasi tukawa mashahidi juu ya ukweli wao unaodumu na sifa zao za kimbinguni zilizojaa nuru.

Tusishangazwe hivyo basi, na rai za baadhi ya walimwengu zinazokwenda kinyume na kanuni ya Allah ya kuwa 'kila nafsi itaonja umauti'; haidhuru iwe ni nafsi ya mpendwa wa Mwenyezi Mungu au kafiri sugu. Yafaa tujaribu kuelewa ya kwamba baadhi yao wameshika rai hii kwa sababu ya kukosa kufahamu hatua zote za safari ya mwanadamu kutoka hadi kufika kwa Allah, Mola wa viumbe vyote. Lakini pia kuna baadhi yao ambao wameshikilia rai hii kwa sababu ya roho zao kutotaka kumnasibishia kifo Nabii wao mpendwa – kama vile Isa wa Nazareti (a.s.) kunako na ndugu Wakristo na baadhi ya Waislam pia. Ukweli kwamba yeye amekufa ilihali atarejea mzimamzima humu duniani, ndicho kitendawili kinachowadumishia huzuni nyoyoni mwao. Sawa na rai yao hii, popote alipo Isa bin Maryam wa Nazareti (a.s.) ni sharti awe yu hai mpaka atakaporejea tena humu ardhini na kusikika tena kauli ya mahubiri yake! Hiki ndicho kilio cha waumini kumlilia Mpendwa wao waliye pokonywa na kifo,na matumaini yao ya kukutana naye tena siku isiyotangazika.

Si hayo tu, bali kipengele kimoja cha rai yao hii kunako na baadhi ya ndugu Waislamu, ni kwamba kwa sababu ya wadhifa wake wa kimbinguni wa kurudi tena humu duniani, ilikuwa ni



Nyumba iliyopo mtaa wa Khanyar Kashmir ambayo ndani yake limo kaburi la mtakatifu - Uchunguzi wa kina wa historia ya mtakatifu huyo inaonesha kwamba kaburi hilo ni la Nabii Isa a.s.

lazima kuahirisha kifo chake kwa muda usiotangazika. Muda huo utakapokwisha na ujaji wake wa mara ya pili kuwadia, ndipo atakapoteremshwa mzimamzima humu duniani; Nabii huyu wa Kitabu cha Injili, kuja kutekeleza majukumu yake yote ya kimbinguni yaliyokuwa yametabiriwa kimbele, ikiwa ni pamoja na kuishindisha dini ya Kiislamu. Haya nayo ni matarajio ya waumini juu ya Nabii wasiyemtakia kifo na matumaini yao ya kukutana naye atakaporejea duniani kwa mara ya pili katika siku isiyotangazika. Rai ya waumini hawa sio tu ya kwamba ni kielelezo cha mapenzi yao juu ya Nabii Isa bin Maryam wa Nazareti(a.s.), bali pia imeadhiriwa pakubwa na msimamo wao dhidi ya kifo sambamba na wanadamu kwa ujumla, kama tulivyotangulia kusema.

Lakini je, kanuni hii ya kifo au mauti, ilivyowekwa na Allah; inayoogopewa na mwanadamu na hata baadhi yao kujaribu kwa karne nyingi kuiepushia kwa Nabii wampendae, Isa bin Maryam wa Nazareti a.s ni kitu kinachoweza kuepukika katika safari ndefu ya mwanadamu tuliyoitaja hapo juu ya kurudi kwa Mola wake? Ili kutupatia fununu ya jawabu la swali sampuli hii, Mwenyezi Mungu Mwenye uwezo juu ya kila kitu Ametupigia muhtasari wa picha ya safari hii ya ajabu ndani ya Neno Lake takatifu Quran tukufu. Akitunasihi dhidi ya majivuno yetu, Mwenyezi Mungu, Mzima wa Milele, Ametamka Akisema: "Mtamkataaje Mwenyezi Mungu hali mlikuwa wafu naye Akawahuisheni, kisha Atawafisheni, kisha Atawahuisheni, kisha Kwake mtarejeshwa?" Safari hii ndefu ya mwanadamu kurudi kwa Mola wake ambayo usafiri wake wanasayansi wameuita "EVOLUTION", yaani safari

Endelea uk. 10